THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSSE) 2020

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2020

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI.......................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI.......................................................................................1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI.......................................................................................2

2.1 SEHEMU A 2

2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi.......................................................................................2

2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha.......................................................................................9

2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi 11

2.2.1 Swali la 3: Historia Katika Uislamu.......................................................................................11

2.2.2 Swali la 4: Qur'an.......................................................................................15

2.2.3 Swali la 5: Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu.......................................................................................17

2.2.4 Swali la 6: Nguzo za Uislamu.......................................................................................21

2.2.5 Swali la 7: Fiqh.......................................................................................25

2.2.6 Swali la 8: Sunnah na Hadithi.......................................................................................29

2.2.7 Swali la 9: Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada........................................................................................33

2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha 35

2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu.......................................................................................35

2.3.2 Swali la 11: Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu.......................................................................................40

2.3.3 Swali la 12: Qur'an.......................................................................................46

2.3.4 Swali la 13: Historia katika Uislamu.......................................................................................52

4.0 HITIMISHO.......................................................................................59

5.0 MAPENDEKEZO.......................................................................................59

Kiambatisho cha Pekee.......................................................................................61

## DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2020 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika somo hili. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Taarifa hii imeweka bayana jinsi ambavyo watahiniwa wameweza kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Sababu zilizochangia baadhi ya watahiniwa kuweza kujibu maswali kwa usahihi zilikuwa, kuelewa vema matakwa ya maswali na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi umebaini kuwa baadhi ya watahiniwa walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kwasababu walikosa ujuzi katika mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kutambua matakwa ya maswali. Uchambuzi umebaini pia udhaifu katika kujenga hoja wakati wa kujibu maswali ya kujieleza kwa ufupi na yale ya kujieleza kwa insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na hatimaye kuondoa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii hivyo kuongeza kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika kipindi kijacho. Baraza la Mitihani linatoa shukran za dhati kwa wote waliohusika katika uandishi wa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imetokana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE). Mtihani huu ulifanyika mwezi Novemba mwaka 2020 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo wa Kidato cha I hadi IV uliotolewa mwaka 2012.

Mtihani huu ulikuwa na karatasi moja iliyokuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na tatu (13). Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2) na sehemu B ilikuwa na maswali saba (7) ya majibu mafupi. Sehemu C ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu tu. Jumla ya alama zote katika karatasi hii zilikuwa 100.

Idadi ya watahiniwa walioandikishwa kufanya mtihani wa Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2020 ilikuwa 70,240. Watahiniwa waliofanya mtihani walikuwa 67,876 (96.63%) sawa na ongezeko la watahiniwa 10,080 (14.85%) ikilinganishwa na watahiniwa 38,996 waliofanya mtihani wa Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2019. Aidha, watahiniwa 67,529 (96.14%) kati ya 67,876 (96.63) walipata matokeo yao. Kati yao watahiniwa 16,864 (24.97%) walifaulu, ambapo hapakuwa na mtahiniwa aliyepata gredi A. Watahiniwa 23 walipata gredi B, 2,069 walipata gredi C na 14,772 walipata gredi D. Watahiniwa 50,665 (75.03%) walipata gredi F. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kwa mwaka 2020 kilikuwa cha wastani ambapo asilimia 32.71 ya watahiniwa walipata alama kati ya gredi B hadi D.

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ambapo sampuli za majibu zimewekwa ili kuonesha kile kilichofanywa. Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika makundi matatu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu ulikuwa dhaifu kama ulikuwa kati ya asilimia 0 hadi 29. wastani kati ya asilimia 30 hadi 64 na mzuri kati ya asilimia 65 hadi 100.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Tathmini ya kila swali imefanyika kwa kuainisha alichotakiwa kufanya mtahiniwa kwa mujibu wa matakwa ya swali, idadi ya watahiniwa waliojibu swali na hali ya ufaulu kwa ujumla katika swali husika.

## 2.1 SEHEMU A

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (1 na 2) yenye alama 20. Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A, B, C, D na E) aliyopewa. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha taarifa zilizo katika orodha A (i) hadi (v) na istilahi (A) hadi (G) zilikuwa katika orodha B. Katika maswali haya kila kipengele kilikuwa na alama moja.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi

Swali la kwanza lilikuwa na vipengele kumi na tano (i) – (xv) vilivyotolewa katika mada za *Sunnah na Hadithi*, *Nguzo za Imani*, *Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini*, *Nguzo za uislamu*, *Qur'an* na *Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w)*. Katika kila kipengele mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo matano aliyopewa kisha kuandika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chake cha kujibia.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 67,866 (100%). Takwimu zimeonesha kuwa watahiniwa 37,889 (55.9%) walipata alama za wastani (5 hadi 8). Watahiniwa 25,989 (38.3%) walipata alama za chini (0 hadi 4) na watahiniwa 3,988 (5.9%) walifaulu vizuri katika swali hili kwa kupata alama kati ya 9 hadi 15. Aidha, mtahiniwa mmoja kati ya waliofaulu vizuri alipata alama zote 15 za swali hili. Chati namba 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao katika asilimia.




**Chati Na. 1**: *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, asilimia 61.7 sawa na watahiniwa 41,877 walipata alama 5 hadi 15. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani. Miongoni mwao asilimia 55.8 walichagua majibu sahihi kwa vipengele 5 hadi 15. Watahiniwa hao walionesha kuwa mahiri katika mada nyingi zilizounda vipengele vya swali, hivyo wengi waliweza kuchagua majibu sahihi katika vipengele vitano au zaidi. Aidha, watahiniwa 3,988 (5.9%) walipata alama za juu (9 hadi 15) kwa kuwa waliweza kuchagua majibu sahihi katika vipengele zaidi ya tisa. Watahiniwa hao waliashiria kuwa na uwezo mzuri katika mada mbalimbali zilizopimwa katika mtihani huu kama ilivyofafanuliwa katika uchambuzi wa kila kipengele ufuatao:

Katika kipengele cha (i) mtahiniwa alitakiwa kuchagua orodha sahihi ya waandishi wa vitabu vya Sahihi Sitta. Watahiniwa mahiri katika historia ya uandishi wa Hadithi wakati wa Tabiin waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi D *Tirmidhy, Annasai, Ibun majah, Abuu Daud, Muslim na Bukhari*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Maimamu hao. Aidha, watahiniwa walioshindwa katika kipengele hiki walichagua kipotoshi E *Tirmidhy, Annasai, Abu Hurayra, Abuu Daud, Muslim na Bukhari* ambacho hakikuwa sahihi kwa sababu ndani yake alitajwa Swahaba *Abu Hurayra*. Wengine walichagua kipotoshi A ambacho hakikuwa sahihi kwa kuwa alitajwa ndani yake *Hambali*. Kipotoshi B hakikuwa sahihi kwakuwa alitajwa *Shafi'i.* Kadhalika kipotoshi C

hakikuwa sahihi kwa kuwa alitajwa Swahaba *Anas bin Malik*. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi walikosa kuwafahamu vema Maimamu sita wa Hadithi pia hawakuweza kujua tofauti kati ya Maswahaba na Maimamu.

Kipengele cha (ii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha vipindi tofauti vya uandishi wa Hadithi za Mtume (s.a.w). Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi A *Uandishi kipindi cha Mtume (s.a.w), Maswahaba, Tabii na Tabii Tabiina*. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume (s.a.w) waliweza kuchagua kwa usahihi jibu hilo. Aidha, vipotoshi B, C, D na E havikutaja vipindi vyote vinne vya uandishi kwa mujibu wa historia ya Hadithi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walivutiwa na majina ya Maswahaba na Maimamu waliotajwa ndani yake bila ya kuzingatia wakati wa uandishi.

Katika kipengele cha (iii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha nafasi ya Bukhari na Muslim wanapotajwa mwishoni mwa Hadithi. Watahiniwa mahiri katika uchambuzi na uhakiki wa Hadithi walichagua herufi ya jibu sahihi B *waandishi wa hadithi*. Watahiniwa wengi waliokosa kipengele hiki walichagu herufi C *Wasimulizi wa Hadithi.* Watahiniwa hawa walichanganya dhana ya sanad na rawi na kuwapa nafasi ya sanad Maimamu hao wawili kutokana na kuathirika na matumizi ya lugha katika kuwaeleza. Aidha, kipotoshi A *Waanzilishi wa Hadithi* hakikuwa sahihi kwa sababu Hadithi za Mtume (s.a.w) si maneno yao bali wao ni waandishi. Vilevile kipotoshi D *Wadhoofishaji wa Hadithi* hakikuwa sahihi kwa kuwa jambo hilo halifafanui nafasi waliyowekwa, kadhalika katika kipotoshi E *Wasanifishaji wa Hadithi* hakikuwa sahihi kwa sababu Hadthi ni nukuu kutoka kwa Mtume (s.a.w) hivyo hairuhusu usanifu.

Kipengele cha (iv) mtahiniwa alitakiwa kubainisha dhana ya kimapinduzi inayolenga kumkomboa mwanaadamu kutoka kwenye giza la ujahili na ukafiri na kumpeleka katika mwangaza wa uchamungu. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika itikadi ya Uislamu kwa ujumla waliweza kubaini jibu sahihi C *Tawhiid*. Watahiniwa hawa walielewa vema itikadi inayobeba falsafa hiyo na dhana zingine katika machaguo ya kipengele hiki. Aidha, baadhi ya watahiniwa walioshindwa katika kipengele hiki walivutiwa na kipotoshi A *Mustalah Al Hadith.* Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kwamba istilahi hiyo ina maana ya *Sayansi ya Hadithi* hivyo, haina falsafa iliyoelezwa katika sentensi ulizi ya kipengele

hiki. Aidha, vipotoshi vilivyobaki B *Tarekh* D *Fiqh* na E *Sira* vilitaja fani zingine za maarifa ya Uislamu ambazo kwa pamoja hazina falsafa iliyoelezwa katika kipengele hiki. *Tarekh* inahusika na historia ya Uislamu kwa ujumla, *Fiqh* inahusika na sheria za Uislamu za kiibada na kijamii, wakati *Sira* inahusu wasifu wa Mtume Muhammad (s.a.w).

Kipengele cha (v) mtahiniwa alitakiwa kubainisha msingi wa upotofu wa tafsiri kuwa "Dini ni imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu muumba". Watahiniwa waliofahamu vema dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu waliweza kutambua jibu sahihi la swali hili kuwa ni B *Mungu si lazima awe Muumba.* Watahiniwa hawa walitambua kuwa siyo wote wenye dini wanaamini kuwepo kwa Mungu na siyo Dini zote zinaamini Mungu muumba bali wengine wanaamini Miungu iliyoumbwa au kutengenezwa. Baadhi ya watahiniwa walichagua kipotoshi C *Haitoshelezi mahitaji* walivutiwa na kipotoshi hicho kwa dhana kuwa Dini ilitakiwa ifafanuliwe zaidi ya hivyo na kushindwa kuelewa kuwa huo ni mtazamo mmoja katika mitazamo mingi ambao ulitakiwa kutajwa udhaifu wake. Wengine walichagua kipotoshi D *Mungu hatambui dini ila Uislamu.* Kipotoshi hiki hakikuwa sahihi kwa kuwa kinapingana na mafundisho ya Qur'an (109:6) ambayo yanatambua uwepo wa Dini zingine. Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi A na E walishindwa kubaini kuwa vilitaja sifa ya tafsiri iliyotolewa katika swali na siyo msingi wa upotofu wake.

Kipengele cha (vi) mtahiniwa alitakiwa kuchagua sababu ya Mwenyezi Mungu kuleta vitabu vya Taurat, Injili na Zaburi. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu waliweza kubaini jibu sahihi la swali hili kuwa ni D *kuwaongoza wanadamu katika njia iliyonyooka* kwani hilo ndiyo lengo lililobainishwa katika vitabu vyote (Qur'an 16:36). Aidha, vipotoshi vyote (A, B, C na E) havikuwa sahihi kwa sababu vilieleza namna mbalimbali ambazo jamii inavitumia kwa sasa kinyume na malengo yake makuu.

Kipengele cha (vii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha tofauti kati ya kuchukua udhu kwa maji na kutayammamu. Watahiniwa mahiri katika sharti la twahara katika Swala waliweza kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua herufi E *Tayammamu inarudiwa kila inavyofika swala nyingine* kwani sifa iliyotajwa hapo ni sahihi na iligusa tofauti sahihi kati yake na kuchukua udhu kwa maji. Aidha, vipotoshi A, B, C, na D havikuwa sahihi kwa kuwa vilitaja sifa ambazo hazitofautishi Tayammam na udhu wa maji.

Kipengele cha (viii) mtahiniwa alitakiwa kubaini mwenendo wa Waislamu unaothibitisha kueleweka vibaya kwa Hadithi inayosema “Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano”. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya nguzo za Uislamu walichagua jibu sahihi D *kutekeleza ibada maalum bila ya kuzingatia athari zake*. Watahiniwa hawa walielewa kuwa Waislamu wenye sifa hiyo wanatosheka kutekeleza nguzo hizo kinadharia bila kujitathmini kulingana na malengo mahususi ya utekelezaji wake. Baadhi ya watahiniwa ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha walichagua kipotoshi C *kutekeleza baadhi ya ibada na kuziacha nyingine* kwa kuwa ni jambo lililozoeleka katika jamii ya Waislamu kufanya hivyo. Hata hivyo, hili halikuwa jibu sahihi kwa mnasaba wa swali kwani waliokusudiwa ni wale wanaotekeleza nguzo zote za Uislamu na kuhisi kuwa wamemaliza wajibu wao katika dini. Aidha, kipotoshi A *kuzipamba ibada zao kwa Sunnah nyingi* na B *kuzitekeleza ibada zote kwa wingi,* havikuwa sahihi kwani hizo sio sifa za watu walioelewa vibaya. Kadhalika, kipotoshi C *kubuni ibada mpya ili kujiongezea uchamungu,* nacho hakikuwa sahihi kwa sababu kilikuwa na sifa ya watu walioelewa vibaya katika dhana ya ibada kwa ujumla.

Kipengele cha (ix) mtahiniwa alitakiwa kubaini hukumu ya mtu aliyeacha kufunga siku moja kwa makusudi. Wanafunzi walioelewa vema Fiqh ya Funga waliweza kubaini jibu sahihi na kuchagua herufi E *hatoweza kuilipa hata kama atafunga kwa mwaka mzima*. Watahiniwa hawa walielewa vizuri ibada ya Funga na nafasi yake katika Uislamu. Watahiniwa wengi walichagua vipotoshi A *atatakiwa ailipe kadha baada ya Ramadhani* na wengine C *atatoa kafara ya ngamia mmoja na kumuacha huru mtumwa* kwa sababu vipotoshi hivyo vilitaja kafara za kawaida kwa makosa mengine. Hata hivyo, hawakuelewa kuwa kwa ujumla hamna kadha inayoweza kufidia kwa ukamilifu siku moja ya Kufunga iliyoachwa kwa makusudi. Aidha, wengine walichagua herufi D *watafunga miezi miwili mfululizo bila kuacha ata siku moja*. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa hiyo ni hukumu mahususi kwa watu waliokutana katika tendo la ndoa mchana wa Ramadhani. Vile vile waliochagua kipotoshi B *Hatoruhusiwa kuendelea kufunga tena siku zitakazobaki,* walishindwa kuelewa kuwa Mwenyezi Mungu huwasamehe waja wake kila wanapotaka kurudi kwake.

Katika kipengele cha (x) mtahiniwa alitakiwa kuchagua jina la Swahaba wa Mtume (s.a.w) aliyekuwa mwandishi wa Qur'an. Watahiniwa mahiri katika historia ya kukusanywa na kuandikwa kwa Qur'an waliweza kutambua jibu sahihi na kuchagua herufi A *Uba'y bin kaab*. Watahiniwa wengi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua herufi C *Anas bin Malik* kwa kuwa ni Swahaba aliyeishi muda mrefu na aliwafundisha watu wengi Qur'an. Hata hivyo, swahaba huyu hakuwa miongoni mwa waandishi wa Qur'an kwa sababu wakati Qur'an inashuka yeye alikuwa mdogo. Wengine walichagua kipotoshi E *Ibn Abbas* kwa kutofahamu kuwa wakati Qur'an inashuka yeye alikuwa mdogo ingawa baadae alikuwa mwanazuoni mkubwa wa Qur'an na tafsiri yake. Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi B *Ammar bin Yasir* na D *Bilal bin Rabaa* walivutiwa na umashuhuri wao  lakini hawakuwa katika waandishi wa Qur'an.

Kipengele cha (xi) mtahiniwa alitakiwa kubainisha tofauti ya msingi baina ya Qur'an na Hadithi. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Qur'an waliweza kujibu kipengele hiki kwa usahihi kwa kuchagua C *Qur'an imekuja neno kwa neno na hadithi imekuja kwa ilham.* Watahiniwa hawa walielewa vema mchakato wa kushuka kwa Qur'an. Watahiniwa walioshindwa kipengele hiki wengine walichagua kipotoshi A *Qur'an ina sura nyingi kulinganisha na Hadith*. Watahiniwa hawa walizifahamu sura 114 za Qur'an lakini walishindwa kujua kuwa hiyo sio tofauti ya msingi baina yake na Hadithi kwa kuwa Hadithi nyingi hazijapangwa katika sura. Aidha watahiniwa waliochagua vipotoshi B na D walishindwa kubaini kuwa vipotoshi hivyo havikuwa na sifa mahususi za Qur'an wala Hadithi, wakati kipotoshi E kilikuwa na sifa za Hadithi pekee.

Kipengele cha (xii) Mtahiniwa alitakiwa kubainisha jozi sahihi inayoeleza vema vituo vyote muhimu katika mchakato wa kushuka Qur'an. Wanafunzi mahiri katika historia ya kushuka kwa Qur'an waliweza kujibu swali hili kwa usahihi na kuchagua A *Lawhim mahfudh-Wingu wa dunia-Jabal hira*. Watahiniwa wengi waliokosa walichagua kipotoshi B *Jabal hira-Lawhim mahfudh-Wingu wa dunia* kwa kuwa Jabal Hira ilikuwa sehemu ya kwanza kwa Mtume (s.a.w) kupokea Qur'an. Jibu hilo halikuwa sahihi kwa sababu liligeuza mpangilio wa vituo vya kushuka kwa Qur'an na Jabal hira ni kituo cha mwisho. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi C *Laylatul-Qadr – Lawhim Mahfudh – Jabal Hira* kutokana na kutajwa Laylatul Qadr ambayo ni maarufu katika historia ya kushuka kwa Qur'an. Jibu hilo pia halikuwa sahihi kwa sababu lilikosa kituo cha pili. Aidha, waliochagua vipotoshi D

na E walishindwa kubaini kuwa vipotoshi hivyo vilichanganya nafasi ya vituo hivyo kutoka katika mpangilio wake.

Katika kipengele cha (xiii) mtahiniwa alitakiwa kuchagua sentensi ambayo ilibainisha madai ya mtume wa uongo Musailama. Watahiniwa mahiri katika historia ya Uislamu walichagua jibu sahihi B *kumiliki nusu ya dunia na nusu nyingine ni ya Maqurayshi*. Watahiniwa hawa waliielewa vema historia ya Musailama na madai yake. Watahiniwa wengine walioshindwa katika kipengele hiki walichagua vipotoshi A, C, na D. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha madai ya Musailama na wengine waliodai utume kama vile Talaiha na Aswad. Aidha, baadhi walichagua kipotoshi E *kumuingiza motoni kila atakayekwenda kinyume na amri ya Allah* (s.w). Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa hoja hii siyo katika madai ya Musailama bali ni ahadi ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Kipengele cha (xiv) mtahiniwa alitakiwa kubaini ishara iliyowaongoza Maswahaba kumchagua Abubakar Swidiq (r.a) kuwa kiongozi wa dola ya kiislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w). Wanafunzi walioifahamu vizuri historia ya Uislamu baada ya kufariki Mtume (s.a.w) waliweza kubaini ishara hiyo na kuchagua jibu sahihi C *kuteuliwa na Mtume* (s.a.w) *kuongoza swala ya jamaa*. Aidha, watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, D na E. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha dhana ya ishara na sifa za kumchagua kiongozi katika Uislamu. Kwani sifa zilizotajwa katika vipotoshi hivyo walikuwa nazo Maswahaba wengi pamoja na yeye Abubakar Swidiq (r.a).

Kipengele cha (xv) mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu kubwa iliyosababisha kuanguka kwa Dola ya kiislamu aliyoiacha Mtume (s.a.w). Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika historia ya Uislamu baada ya kufariki Mtume (s.a.w) walijibu kipengele hiki kwa kuchagua herufi C *kugombana waislamu wenyewe kwa wenyewe.* Watahiniwa hawa walielewa vema athari za mgogoro uliojitokeza baina ya Maswahaba (r.a) na matokeo yake. Aidha, watahiniwa wengi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua kipotoshi D *Imani dhaifu ya waumini wa dini ya kiislamu.* Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa hoja hiyo ilisababisha kutokea kwa uasi baada ya kufariki Mtume (s.aw) hali ambayo ilidhibitiwa mapema. Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B na E walishindwa kujua kuwa hoja hizo hazikuwa na nguvu tena baada ya kusimama kwa dola ya Kiislamu.

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali hili lilitoka kwenye mada ya Nguzo za Uislamu mada ndogo ya Kusimamisha Swala. Mtahiniwa alitakiwa kuoanisha tafsiri tano za kifiqh (i) - (v) kutoka orodha A na istilahi sahihi (A) hadi (G) kutoka orodha B.

Watahiniwa 67,812 (99.9%) walijibu swali hili. Kati ya hao watahiniwa 30,026 (44.3%) walipata alama za wastani (2 hadi 3). Watahiniwa 24,978 (36.8%) walipata alama za chini (0 hadi 1) na watahiniwa 12,808 (18.9%) walifaulu vizuri na kupata alama kati ya 4 hadi 5. Miongoni mwao, watahiniwa 4,865 (7.2%) walipata alama zote 5 katika swali hili. Chati namba 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, asilimia 63.2 sawa na watahiniwa 42,834 walipata alama 0 hadi 1.5. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani. Watahiniwa 4,865 (7.2%) kati ya waliofaulu vizuri walipata alama zote 5. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika Fiqh ya Swala na waliweza kutumia vema maarifa yao kuoanisha tafsiri na istilahi zake kwa usahihi.

Aidha, asilimia 36.8 ya watahiniwa walipata alama za chini (0 na 1). Watahiniwa hawa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika ibada ya Swala. Hivyo, walishindwa kubaini majibu sahihi. Kati ya hao watahiniwa 8,784 sawa na asilimia 12.9 walipata alama 0 baada ya

kushindwa kuoanisha kwa usahihi tafsiri na istilahi husika katika kipengele (i) hadi (v). ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele.

Katika kipengele cha (i) mtahiniwa alitakiwa kubaini wito unaoashiria kusimama kwa ibada ya Swala. Watahiniwa mahiri katika utekelezaji wa ibada ya Swala walielewa vema matakwa ya kipengele hicho na kuoanisha kwa usahihi kwa kuchagua herufi F *Iqama*. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki wengi walichagua herufi G *Adhana.* Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa *Adhana* ni *Wito unaoashiria kuwadia kwa wakati wa Swala* na sio *kusimama kwa ibada ya Swala.* Watahiniwa wengine walichagua herufi C *Takbirat Ihram* kwa kuwa ndiyo kauli ya mwisho kabla ya kuanza kuswali. Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa *Takbirat Ihram* ni kifunguzi cha Swala, inaposomwa inamaanisha kuanza kwa ibada yenyewe na kuwataarifu waumini kujihudhurisha ndani ya ibada.

Kipengele cha (ii) mtahiniwa alitakiwa kubaini Sunnah inayoswaliwa baada ya kuchomoza jua na kabla ya mchana. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika Swala za Sunnah waliitambua ibada hiyo na kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi E *Dhuha*. Ama watahiniwa waliofeli kipengele hiki walichagua herufi A *Qabliya*, kwa kuwa ni Swala maarufu katika Sunnah. Hata hivyo, uchaguzi huo haukuwa sahihi kwa sababu Qabliya ni Swala ya Sunnah inayotekelezwa muda mfupi kabla ya swala za faradh tofauti na muda uliotajwa katika swali.

Kipengele cha (iii) mtahiniwa alitakiwa kubaini tafsiri ya nguzo ya matamshi katika swala. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya nguzo za Swala waliweza kuchagua jibu sahihi B *Tashahud.* Watahiniwa hao walibaini kuwa jibu hilo ni sahihi katika nafasi hiyo baada ya kuelewa vizuri tafsiri zilizobaki. Aidha, wathiniwa wengi walioshindwa kipengele hiki walichagua herufi F *Iqama* kwakuwa inasomwa kwa sauti kabla ya kuanza kuswali. Wanafunzi hawa walishindwa kubaini kuwa Iqama siyo nguzo ya swala bali ni Sunnah.

Katika kipengele cha (iv) mtahiniwa alitakiwa kubaini istilahi inayotumika kuhusu kifunguzi cha ibada ya Swala. Watahiniwa wenye maarifa ya kutosha kuhusu utekelezaji wa ibada ya Swala waliweza kufahamu jibu sahihi na kuchagua herufi C *Takbiratul Ihram*. Aidha, watahiniwa wengi walioshindwa walichagua jibu F *Iqama* kwa kuwa inaposomwa watu

husimama na kujipanga katika safu kujiandaa kuanza kuswali. Watahiniwa hawa hawakuelewa tafsiri ya *Iqama* ambayo ni *wito unaoashiria kusima kwa ibada ya Swala* kwa malengo ya kuwaweka waumini tayari kwa ajili ya kuanza kuswali na siyo kufungua Swala. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nafasi ya Iqama katika ibada ya Swala.

Katika kipengele cha (v) mtahiniwa alitakiwa kubaini maji ya asili yanayofaa kujitwaharishia. Watahiniwa mahiri katika sharti la kwanza la Swala (twahara) walitambua maji hayo na kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua D *Mutlaq*. Watahiniwa wengine walijibu kipengele hiki kwa kuchagua kipotoshi E Dhuha. Uchaguzi wa jibu hilo ulidhihirisha kwamba hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ibada ya Swala kwa ujumla, kwani Dhuha ni aina ya Swala ya Sunnah na siyo maji.

## 2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi. Maswali hayo yalitoka mada za *Historia katika Uislamu*, *Qur'an, Mtazamo wa uislamu juu ya Elimu*, *Nguzo za Uislamu*, *Fiqh*, *Sunnah na Hadithi* na *Mtazamo wa Uislamu juu ya ibada.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, kila swali lilikuwa na alama tano (5) hivyo jumla ya alama zote zilikuwa 35.

### 2.2.1 Swali la 3: Historia Katika Uislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kulinganisha makosa mawili ya watu wa Nabii Lut na yale yanayofanyika katika zama hizi. Watahiniwa 63,615 (93.7%) kati ya 67,867 (100%) walifanya swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 40,040 (62.9%) walipata alama za chini (0 hadi 1.5). Watahiniwa 20,235 (31.8%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 2,340 (5.3%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, asilimia 62.9 sawa na watahiniwa 40,040 walipata alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao watahiniwa 28,571 (42.1%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu. Baadhi ya watahiniwa hao waliacha kujibu swali hili na wengine walishindwa kujibu ipasavyo kutokana na sababu mbalimbali kama zilivyobainishwa katika uchambuzi wa majibu ya watahiwa ufuatao:

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 katika swali hili walijibu kinyume na matakwa ya swali husika. Watahiniwa hawa walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika historia ya Mitume walioteuliwa. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza tabia za watu wa Nabii Shuayb badala ya Nabii Lut (a.s) kama vile: *Kupunguza vipimo wakati wa kuwapimia watu.*

Watahiniwa wengine walitofautisha sifa za waumini wa Nabii Lut (a.s) na waumini wa sasa hivi badala ya kulinganisha makosa ya watu wa Nabii Lut (a.s) na yanayofanywa katika zama hizi, watahiniwa hao walieleza kuwa: *Watu wa Nabii Lut walikuwa likitajwa jina la Allah wanapata khofu moyoni lakini zama hizi hakuna amuogopae Allah na Watu wa Nabii Lut walihofishwa na adhabu za Allah lakini zama hizi waja hawaogopi adhabu zake.* Aidha, watahiniwa wengine walibuni makosa ambayo hayakufanyika katika zama za Lut (a.s) na kuyalinganisha na sasa, mfano wa makosa hayo yalikuwa: *Watu wa Nabii Lut (a.s) walikuwa hawapendi kufanya ibada ni*

*sawa na watu wa zama hizi na Watu wa nabii Lut walikufuru chakula pia walipenda kufanya israfu ya chakula sawa na watu wa zama hizi za leo nao pia hupenda kufanya israfu sana.*

Watahiniwa wengine walitofautisha tabia za watu wa Nabii Musa (wana wa Izraeli) na watu wa zama hizi. Badala ya watu wa Nabii Lut na watu wa zama hizi, nao waliandika hoja zifuatazo: *Watu wa Nabii Lut walitaka kumuona Allah (s.w) kwa madai ya kuwa wanataka kumshuhudia ni jinsi gani alivyo vile vile wanaadamu wa sasa wanataka kumuona Allah kwa madai ya kuwa hawatoamini juu ya uwepo wa Allah mpaka watakapo muona na Watu wa Nabii Lut walifanya kosa la kutoamini juu ya uwepo wa Allah (s.w) na pia wanaadamu wa zama hizi wanafanya kosa la kutoamini juu ya uwepo wa Allah (s.w).*

Watahiniwa hao wote walienda kinyume na matakwa ya swali ambayo yalibainishwa wazi katika sentensi ulizi. Hali hii pia ilisababishwa na kukosa maarifa ya kutosha katika historia ya Mitume waliopita. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.


3. Kulinganisha makosa mawili yawatu wa Nabii Lut nayo le yanayo fanyika katika zama hizi
(i) Zama za nabii Luti walikuwa hawamwamini Mwenyezi mungu nakufanya maovu
(ii) Zama za sasa wanaamini kuwepo kwa Mwenyezi mungu

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali la 3

Kielelezo namba 3.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alijibu kinyume na msingi wa swali. Hivyo basi alishindwa kujenga hoja zinazotaja makosa ya kaumu ya Nabii Lut (a.s) na kufanya ulinganifu katika zama zetu. Badala yake alieleza sifa ya jumla ya watu wa Lut na sifa ya jumla ya watu wa zama hizi.

Watahiniwa waliofaulu (37.1%) katika swali hili na kupata alama 2 hadi 5 walitambua vema matakwa ya swali na kuweza kutumia maarifa yao kujibu kama lilivyokusudiwa. Aidha, kati yao (31.8%) walipata alama za wastani

(2 hadi 3.5). Watahiniwa hao baadhi walitaja makosa sahihi ya watu wa Nabii Lut (a.s) lakini walishindwa kulinganisha makosa hayo na yale yanayofanywa na watu wa zama hizi. Wengine waliweza kutaja na kueleza kosa moja pekee na kulinganisha kosa hilo kwa usahihi na yale yanayofanywa katika zama hizi. Hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa waliopata alama za juu (4 hadi 5) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya historia ya Nabii Lut (a.s) na kaumu yake, na walielewa vema matakwa ya swali hivyo kujibu kwa ufasaha. Makosa ambayo yalibainishwa na watahiniwa hawa ni: (i) *Walikuwa wakiwaendea wanaume wenzao katika kutosheleza matamanio yao, jambo ambalo linafanyika pia katika zama hizi,* (ii) *Walikuwa wanafanya uharamia na uporaji wa mali za watu jambo ambalo katika zama hizi tunashuhudia yakifanyika,* (iii) *Walikuwa wakifanya makosa yao waziwazi (bila ya kificho) kama ambavyo leo hii kwenye jamii yetu yanavyofanyika*, na (iv) *Hawakuwa watiifu kwa viongozi wao kama ambavyo jamii ya sasa inafanya*. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


3. i) Kuingiliana jinsia moja katika enzi za Na-
bii Lut wanaume walikuwa wakiingiliana wao-
kwa wao kutosheleza mahitaji yao na hata-
sasa hivi kuna wanaume na wanawake weng-
i wanaoingiliana jinsia moja.

ii) Kupora na kudhulumu mali za watu. enzi
za Nabii Lut watu walikuwa wakipora mali
za watu na kuwadhulumu na hata katika jamii-
ya sasa kuna watu wengi wanaodhulumu na-
kupora mali za watu

Kielelezo Na. 3.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 3

### 2.2.2 Swali la 4: Qur'an

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuchambua faida mbili anazoweza kuzipata kwa kuanza kila jambo jema kwa *Bismillahir Rahmanir Rahiim.* Watahiniwa 67,200 (99.0%) walifanya swali hili. Kati ya hao watahiniwa 38,259 (56.9%) walipata alama za chini (0 hadi 1.5), 24,685 (36.7%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 4,256 (6.3%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na.4:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 56.9 sawa na watahiniwa 38,259 walipata alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao wanafunzi 13,177 (19.6%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu. Baadhi ya watahiniwa hawa waliacha kujibu swali hili na wengine walishindwa kujibu ipasavyo kutokana na sababu mbalimbali kama ilivyofafanuliwa katika uchambuzi ufuatao wa majibu ya watahiniwa.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili waligawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza walichanganya dhana ya Basmallah na Isti-a'zat. Watahiniwa hawa badala ya kuelezea faida za *Bismillahir Rahmanir Rahiim* walieleza faida za *Audhubillah_Mina*

*Shaitwan_Rajiim* ambazo ni: *Kujilinda na Shetani aliyelaaniwa na Kumuondoa Ibilisi katika mambo yako*. Majibu haya yaliashiria kuchanganya baina ya dhana hizo mbili tofauti.

Kundi la pili walishindwa kuelewa vema swali husika, Baadhi yao walitafsiri maana ya maneno *Bismillahir Rahmanir Rahiim* badala ya kutoa faida zake, watahiniwa hawa waliandika: *Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na mwenye kurehemu*. Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa vema matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa wengine walioshindwa kuelewa swali hilo, walifafanua kila neno moja kipekee katika muungano wa maneno hayo matatu na kujibu kwa ujumla kuwa: *Hayo ni miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu.* Badala ya kuchambua faida zake kama walivyoulizwa katika swali la msingi. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


4. Kuchambua faida mbili unazoweza kuzipata kwa kuanza na kila jambo jema kwa Bismillahir Rah manir Rahiim

(i) Unajiepushana sheitwani kwa kuanza na Bismilah Rah man rahiim

(ii) Unajilinda na sheitwani kwa kutaja Bismilahi

Kielelezo Na. 4.1 Sampuli majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 4

Kielelezo namba 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alichanganya dhana ya *Basmallah* na ile ya *Isti-a'zat* na kueleza faida za kusoma *Audhubillah Mina Shaytwan Rajiim* badala ya *Bismillahir Rahmanir Rahiim.*

Watahiniwa (43.0%) waliofaulu katika swali hili na kupata alama 2 hadi 5 walielewa vema matakwa ya swali na walitumia maarifa yao vizuri kujibu swali hilo. Aidha, asilimia 36.7% kati yao walipata alama za wastani (2 hadi 3.5). Watahiniwa hawa baadhi yao waliorodhesha faida sahihi bila kuzifafanua kwa ufupi. Wengine walitoa faida moja pekee na kuichambua vizuri, hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa waliopata alama za juu (4 hadi 5) ambao ni asilimia 6.3 walionesha kuwa na ujuzi wa kutosha katika mafunzo ya Qur'an kwani waliweza kuchambua kwa ufasaha faida za kuanza kila jambo jema kwa *Basmallah.* Watahiniwa hao walieleza faida zifuatatazo: (i) *Kuomba msaada kwa Allah ili alifanikishe jambo tunalolifanya,* (ii) *Kujikinga na maovu au maasi,* (iii) *Humzoesha muumini kubaki katika ibada katika kila kipengele cha Maisha yake na* (iv) *Kupata baraka katika jambo tunalolifanya.* Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi yaliyotolewa na mtahiniwa katika swali hili.


4 Bismillahir-rahamanir-rahiim maana yake
ni kuomba kwa jina la mwenyezimungu mwingi
wa rehema mwenye kurehemu. ni muhimu kwa
muislamu pindi anapoliendea jambo lake kuanza
na bismillahi Rahamani Rahiim kwa sababu
Unakuwa katika Ulinzi wa Allah, Unapo
sema bismillahi Unakuwa katika Ulinzi wa Allah
na shetani hana nafasi hivyo kupelekeo kufani
kisha katika jambo lako.
Kutambuo na kukumbuko Uwepo wa
Allah, lakini pia kabla yo kuliendea jambo lako
lako Unaposema bismillahi Allah anakusimamia
kwani Umethamini na kukumbuka Uwepo wake.

Kielelezo 4.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 4

### 2.2.3 Swali la 5: Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi namna mbili za kuigawa elimu zinazokubalika katika Uislamu. Watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 63,181 (93.1%) kati yao watahiniwa 53,542 (84.7%) walipata alama za chini (0 hadi 1.5). Watahiniwa 6,352 (10.1%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 3,287 (5.2%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao.




**Chati Na. 5:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, asilimia 84.7 sawa na watahiniwa 53,542 walipata alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao wanafunzi 49,227 (72.9%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu. Ufaulu huo umesababishwa na baadhi ya watahiniwa hao kuacha kujibu swali hili na wengine kujibu kinyume na matakwa ya swali. Aidha, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umebaini yafuatayo:

Mosi, watahiniwa wengi waliopata alama za chini katika swali hili walikosa ufahamu sahihi katika dhana ya mgawanyo wa elimu kwa mtazamo wa Uislamu. Jambo hilo limedhihirika kutokana na aina ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao. Miongoni mwao waliigawa elimu katika mtazamo unaopingana (kinyume) na Uislamu ambao ni *Elimu ya akhera na Elimu ya Dunia*, wengine walizitaja kama *Elimu ya akhera na Elimu ya kisekula*. Watahiniwa hao waliashiria kuathirika na maoni ya kijamii yaliyotokana na dhana potofu ya kuyagawa maisha kidunia na kidini.

Pili, wengine walieleza mgawanyo wa elimu katika makundi ya *Elimu yenye manufaa na Elimu isiyo na Manufaa*, mgawanyo huu haupingani na Uislamu, lakini hautoshi kujibu swali hili kwa kuwa siyo mahususi kwa mujibu wa Qur'an (2:31 na 38) ambazo zimeeleza dhana ya elimu. Hivyo, mgawanyo huo hautoshi kufafanua makundi makuu ya elimu.

Tatu, watahiniwa waliokosa maarifa katika dhana ya elimu katika mtazamo wa Uislamu walieleza mgawanyo huo kuwa *Elimu ya hiari na Elimu ya lazima*, mtazamo ambao siyo sahihi kwa sababu elimu kwa ujumla ni *Faradh* (lazima). Baadhi waliandika: *Elimu ya kiislamu na Elimu ya kikristo* majibu ambayo yalidhihirisha kukosa maarifa ya kutosha juu ya dhana ya mgawanyo wa elimu kwa mujibu wa Uislamu.

Mmoja wa watahiniwa walioshindwa kuelewa matakwa ya swali alieleza aina za haki badala ya mgawanyo wa elimu, kama vile *Haki ya kuabudu na Haki ya kuishi.* Mwingine alieleza faida ya elimu kama vile *Kuondoa mgongano wa kielimu kutokana na baadhi ya watu kutojua mambo gani yanayotokana na Elimu gani na kuikuza Elimu*.

Watahiniwa wengine walieleze makundi ya dini kwa mtazamo wa Uislamu badala mgawanyo wa elimu. Watahiniwa hao walijibu *Dini ya Allah (Al-islamu) na Dini za watu (Ukafiri, Ushirikina, Utawa).* Kutokana na majibu haya watahiniwa walipata alama za chini na wengine walipata alama 0. Kielelezo namba 5.1 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali na hatimaye kupata alama 0.



5 Namna za kugawanya Elimu juu ya Uislamu.

(i) Mgawanyo wa Elimu juu ya Elimu ya dunia hii inamaanisha kwamba Elimu ya aina hii inajikita kwenye mafanikio ya kidunia mfano Nyumba, Magari, Mali na hata watoto: ambayo imetolewa kwa ajili ya kuashiria kuwa Elimu ya dunia huna ona kwamba maisha ya hapa duniani

(ii) Mgawanyo wa Elimu juu ya Elimu Akhera. hii inaonesha mwanadamu kuutoa mwili wake sadaka duniani ili aweze kumtumikia mungu sababu mbinguni kunamaisha marefu tena ya milele ila duniani tunakufa ila hii Elimu inamuonesha mja kujitakasa na kuweza kuona ufalme

Kielelezo Na. 5.1 Sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi katika swali la 5

Watahiniwa 9,639 (15.3%) walifaulu katika swali hili na kupata alama kuanzia 2 hadi 5. Watahiniwa hawa walielewa matakwa ya swali na kutoa hoja sahihi zinazobainisha mgawanyo wa elimu unaokubalika katika Uislamu. Aidha, watahiniwa 6,352 (10.1%) waliopata alama za wastani (2 hadi 3.5) walitaja mgawanyiko huo kwa usahihi lakini hawakufafanua majibu yao. Wengine waliweza kutaja kundi moja na kulifafanua kwa usahihi na kukosa kundi lingine hatimaye watahiniwa hao walipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine watahiniwa 3,287 (5.2%) walipata alama za juu (4 hadi 5) katika swali hili. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya elimu kwa mujibu wa Uislamu. Hivyo, waliweza kutoa mtazamo sahihi juu ya namna elimu ilivyogawanywa na kufafanua majibu yao kwa ufasaha. Watahiniwa hao walitaja mgawanyiko huo kuwa ni *Elimu Faradh A'in (Elimu ya Muongozo) na Elimu faradh Kifaya (Elimu ya Mazingira).* Kielelezo Na 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



5. i) Elimu ya Muongozo.
Hii ni elimu ambayo kila mja hupaswa kuwa nayo ili kuweza kujua Allah (s.w) ipasavyo na kukiondea kila kipengele cha maisha ya kila kwani Allah ndiye mmiliki wa ulimwengu wote, hivyo inawezesha kupata muongozo juu ya maisha ya hapa duniani na akhera Mfano:- Kuswali, Kutoa zakhat

ii) Elimu ya Mazingira
Hii ni elimu ambayo humuwezesha mja kukiondea kila kipengele cha maisha yake ya kila siku katika kukidhi haja katika mazingira yanayomzunguka kila siku. Mfano kusoma vitabu, kujua na kuweza kupanga kazi mbalimbali.

Kielelezo 5.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 5

### 2.2.4 Swali la 6: Nguzo za Uislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutofautisha kwa hoja tano baina ya Zakat ya mali na Zakatul Fitri. Watahiniwa 63,528 (93.6%) kati ya watahiniwa 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 53,647 (86.6%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 9,251 (12.4%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 915 (1.4%) pekee ndio walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao.




**Chati Na 6:** *Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 6.*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 86.6 sawa na watahiniwa 53,647 walitapa alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao asilimia 59.5 walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawa waliacha kujibu swali hili na wengine walishindwa kujibu kwa usahihi kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Zakat. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umebainisha kama ifuatavyo:

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa wengi waliopata alama za chini katika swali hili walikosa maarifa ya kutosha katika dhana ya Zakat kwa ujumla. Hivyo, walishindwa kuunda vigezo vinavyoweza kutofautisha baina ya Zakat ya mali na Zakatul Fitri.

Baadhi ya watahiniwa walitumia kanuni za utoaji katika Uislamu kwa ujumla na kuziandika upande wa Zakat ya mali kisha kuandika kinyume chake upande wa Zakatul Fitri. Watahiniwa hao walieleza kuwa; (i) *Zakatul mali hutolewa kati na kati lakini zakatul fitr haitolewi kwa kati na kati,* (ii) *Zakatul mal hutolewa vilivyo halali wakati zakatul fitr haitolewi vilivyo halali,* (iii) *Zakatul mal hutolewa vilivyo vizuri lakini zakatul fitr hutolewa visivyo vizuri,* (iv) *Zakatul Mali hutolewa kwa kujiepusha na ria au masimbulizi lakini Zakatul fitr hutolewa kwa ria au masimbulizi.* Majibu

hayo hayakuwa sahihi kwa kuwa hayatofautishi baina ya dhana hizo mbili, pia yanapingana na ukweli kuhusu Zakatul Fitri.

Wengine walijenga hoja ambazo hazina asili katika Uislamu kujibu swali hili. Miongoni mwa hoja zilizotolewa ni kama vile; (i) *Zakatul mali inatolewa pale ambapo mtu hana vitu na yeye hufidia kutoa mali na zakatul fitr inatolewa kwa kutoa vitu ambavyo ni vya thamani*, (ii) *Zakatul mali inatolewa kwa watu na kupelekewa mkuu wa msikiti aigawe kwa maskini na zakatul fitr hii mtu mwenyewe anampelekea anayehitaji*, (iii) *Zakatul mali inatolewa kwa fidia ya kibaba lakini zakatul fitr inatolewa kwa kibaba*. Hoja zote ziliashiria kutofahamika kwa dhana ya Zakat miongoni mwa watahiniwa. Hivyo walipata alama 0.

Mtahiniwa mmoja alijibu kuwa: (i) *Zakatul mali hutolewa wakati wa mazishi na zakatul fitr hutolewa baada ya Ramadhan*, (ii) *Zakatul fitr lengo lake ni kumtolea marehemu lakini Zakatul mal kufikisha funga ya mtu,* (iii) *Zakatul Mali hutolewa kila itakapotokea msiba lakini zakatul fitr hutokea kwa mwaka,* (iv) *Zakatul mali hutoa ndugu wa marehemu lakini zakatul fitr hutoa mfungaji mwenyewe na* (v) *Zakatul mal haina watu maalumu lakini zakatul fitr ina kiwango na inapewa kwa watu maalumu*. Majibu haya yaliashiria kukosa maarifa kuhusu Zakat. Hivyo mtahiniwa aliandika vigezo ambavyo havikuwa sahihi katika kutofautisha dhana hizo.

Aidha, mtahiniwa mwingine alijibu kuwa: (i) *Zakatul mali hutolewa popote pale, Zakatul Fitri hutolewa msikitini na siku ya Idi el fitri.* (ii) *Zakatul mali haina kiwango maalumu, Zakatul fitri ina kiwango maalum* (iii) *Zakatul mali unampa yoyote unaemtaka, Zakatul fitri wanapewa wanaostahili kupewa.* (iv) *Zakatul mali inatolewa muda wowote unaotaka, Zakatul fitri ina muda na siku maalumu.* (v) *Zakatul mali wanapewa watu wowote, Zakatul fitri wanapewa mafukara, masikini na mayatima.*

Majibu hayo ya watahiniwa yalidhihirisha kutokuwa na maarifa katika dhana ya Zakat, hivyo walijibu kutokana na mitazamo yao binafsi ambayo haikuwa sahihi. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 6.



| 6. | Zakat ya mali | Zakatul Fitri |
|---|---|---|
| 1. | Hutolewa na familia ya Waislamu kama vile ukoo ~~and~~ au ndugu | hutolewa na mtu mmoja. |
| ii. | Hutolewa kwa kiasi kikubwa | Hutolewa kulingana na mali zilivyo |
| iii | Kama ni ngombe 100 hutolewa ngombe 40 kama zakat | Inategemea na Mahitaji |
| iv | Inatolewa kipindi cha njaa na shida | Hutolewa kipindi chochote. |
| v | Ina swawabu nyingi sana | Ina swawabu semg hamshindi ya kwanza kwa uwingi |

Kielelezo Na. 6.1 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 6.

Watahiniwa 10,166 (13.9%) waliofaulu katika na kupata alama kuanzia 2 hadi 5 walifahamu vigezo sahihi vinavyotofautisha baina ya Zakat ya mali na Zakatul Fitri. Hivyo, waliweza kubainisha kuanzia vigezo viwili hadi vitano. Aidha, watahiniwa 9,251 (12.4%) kati yao walipata alama za wastani (2 hadi 3.5), kwa kuwa waliweza kubaini na kufafanua kwa ufupi vigezo viwili hadi vitatu na kushindwa vingine hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa 915 (1.4%) waliopata alama za juu (4 hadi 5) katika swali hili, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Zakat kwa ujumla. Watahiniwa hao walibaini vigezo sahihi vinavyotofautisha Zakat ya mali na Zakatul Fitri na kuvifafanua kwa ufasaha. Vigezo hivyo ni: (i) *Zakat ya Mali nisaab yake inategemmea aina ya mali wakati zakatul Fitr nisab yake ni pishi moja(2.5 kg),* (ii) *Zakatul Mali ni lazima kwa mwenye kumiliki mali tu na si pamoja na wanaomtegemea wakati zakatul fitr inamlazimu mkuu wa familiya na wote walio chini yake kulingana na uwezo wake wa*

*kiuchumi,* (iii) *Zakatul mali kiwango cha kutolewa ni maalum kutegemea na aina ya mali au zao wakati zakatu fitr kiwango cha kila kichwa ni sa'i au pishi moja ambayo ni sawa na kilo mbili na nusu,* (iv) *Zakatul mali hutolewa baada ya mali iliyofika nisaab kupindukia mwaka au baada ya mavuno wakati zakatul fitr hutolewa baada ya kukamilishwa kwa funga ya Ramadhani na kabla ya kuswaliwa kwa swalatul iddul fitr,* (v) *Zakatul Mali ni nguzo ya tatu katika uislamu lakini zakatul fitr sio nguzo katika uislamu.* Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.



| 6 | Tofauti ya | |
|---|---|---|
| | Zakatul mali | Zakatul Fitri |
| | - Huhusisha utoaji wa kila mali | - Huhusisha utoaji wa chakula kwa ajili ya iddi |
| | - Ni nguzo ya Uislamu | - ni Sunnah iliyo kokotezwa |
| | - Hutolewa baada ya mwaka kupita | - Hutolewa kabla ya kuswaliwa kwa swala ya eid el fitr na baada ya mwandamo |
| | - Ina kiwango kikubwa cha utoaji | - Huhusisha utoaji wa kiwango kidogo cha chakula kwa ajili ya eid |
| | - Mtu hutoa mali yake mwenyewe kwa niaba yake | - Mtu huwatolea watu wote ambao wako chini ya uangalizi wake |

Kielelezo namba 6.2 Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 6

### 2.2.5 Swali la 7: Fiqh

Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b), katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kutoa maana ya Fiqh na kipengele (b) alitakiwa kuonesha jinsi misingi mitatu ya Fiqhi inavyotegemeana. Watahiniwa 62,090 (91.5%) kati ya 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu walijibu swali hili.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 47,403 (76.3%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 12,863 (20.7%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 1,824 (3.0%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, asilimia 76.3 sawa na watahiniwa 47,403 walitapa alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao watahiniwa 25,899 (38.2%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu. Baadhi ya watahiniwa hao waliacha kujibu swali hili na wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha katika Fiqh. Hivyo walishindwa kubainisha kwa ufasaha maana na misingi yake. Uchambuzi ufuatao unafafanua zaidi sababu za watahiniwa hao kushindwa:

Katika kipengele (a) baadhi ya watahiniwa waliandika maana mbalimbali za Fiqh kulingana na vile walivyofikiria. Baadhi yao waliandika kuwa: *Fiqh ni msingi wa swala ili kumpwekesha Allah (s.w).* Wengine wakaandika: *Fiqhi ni kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye giza la ujahili na ukafiri na kumpeleka katika muongozo wa uchamungu*. Wengine waliandika: *Fiqh ni kumfuata Allah (s.w) na Mtume wake katika kila jambo jema ambalo Mtume (s.a.w) amefanya katika Uislamu.* Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutasha kuhusu dhana ya Fiqh.

Wapo watahiniwa waliofafanua dhana ya Fiqh kwa kueleza umuhimu au miongoni mwa kazi zake, kama vile: *Fiqh ni somo linalofundisha juu ya kutekeleza ibada*. Wengine wakaeleza: *Somo la Fiqhi hutufundisha kuwa ibada imeletwa kwa Waislamu ili kujitoa katika giza kuondokana na machafu na kutupeleka katika nuru*. Maelezo ambayo yanagusa dhana ya

Fiqh kwa ujumla lakini hayakuwa majibu mahususi kufafanua dhana hiyo. Hivyo yalidhihirisha kuwa watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Fiqh.

Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kuonesha jinsi misingi mitatu ya Fiqhi inavyotegemeana. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo walieleza faida za Fiqhi kama vile: (i) *Fiqhi hutufundisha kutekeleza ibada tofauti kama ibada ya kuhiji, kufunga na kuswali*, (ii) *Fiqhi huwafundisha waislamu kuachana na machafu* na (iii) *Fiqhi hutufundisha kuwa ibada imeletwa kwa waislamu ili kujitoa katika giza kuondokana na machafu na kutupeleka katika nuru.* Watahiniwa hawa walionesha kuelewa vibaya swali ambalo lilihitaji misingi ya Fiqh badala ya umuhimu wake.

Watahiniwa wengine walieleza aina za Fiqhi na kuchanganya na dhana ya Tawhiid. Watahiniwa hawa walijibu kuwa: *Fiqhi imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni Fiqhi muamalat, Fiqhi ibadat na Fiqhi asmaa-waswifat*. Mwingine akaeleza kama: *Fiqhi ya maswali na Majibu, Fiqhi ya mambo mahususi na Fiqhi ya mambo katika uislamu*. Mwingine akaitaja misingi hiyo kuwa ni: *Kusoma Qur'an na Hadithi, Kumcha Mwenyezi Mungu na kufuata yale yote aliyoamrisha Mwenyezi Mungu.*

Majibu ya watahiniwa hawa yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana Fiqh kwa ujumla. Hivyo hawakuweza kutoa majibu stahiki ya swali. Kielelezo Na. 7.1 kimeonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


7 a. Fiqh: Ni kipawa cha mwanaadamu am
bacho mtu anatakiwa nacho.
b. (i) Fiqh ibadat: Hii ni fiqh kwa ajili ya ibada.
(ii) Fiqh muamalat: Hii ni fiqh ya waam
ala kwa watu wote.
(iii) Fiqh asmao wasifat.

Kielelezo 7.1 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 7

Watahiniwa 14,687 (23.7%) walifaulu katika swali hili na kupata alama kuanzia 2 hadi 5. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Fiqh na waliweza kufafanua dhana hiyo na kubainisha misingi yake. Kati yao asilimia 20.7 walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) kwa kuwa baadhi yao waliweza kutoa maana ya Fiqh na kutaja misingi yake lakini walishindwa kuonesha jinsi misingi hiyo inavyotegemeana.

Aidha, watahiniwa 1,824 (3.0%) waliopata alama za juu (4 hadi 5) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Fiqhi. Watahiniwa hao walifafanua dhana hiyo kwa ufasaha na kubainisha jinsi misingi yake mitatu inavyotegemeana. Watahiniwa hawa walieleza maana ya Fiqh kuwa: *Kilugha neno Fiqhi lina maana ya ufahamu juu ya jambo fulani, Kisheria ni taaluma au fani inayohusiana na ufahamu juu ya maamrisho na makatazo ya Allah (s.w) ya kibinafsi au ya kijamii ili yaweze kutekelezeka*. Katika kipengele cha pili (b) watahiniwa hao walibainisha namna misingi mitatu ya Fiqhi inavyotegemeana kama ifuatavyo: *Qur'an hubainisha maamrisho na makatazo mbalimbali katika Maisha ya kibinafsi na kijamii ya mwanaadamu kama yalivyotolewa na Allah (s.w) kwenda kwa Mtume (s.a.w), Sunnah ni mwenendo na mafundisho ya mtume(s.a.w) katika kuitafsiri Qur'an, Ijtihad ni juhudi za maswahaba wa Mtume (s.a.w) na wanazuoni katika kufafanua sharia zilizomo katika Qur'an na Sunnah kwa mujibu wa wakati uliopo.* Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyejibu katika swali hili.


7. a) Fiqh, ni fani ya elimu ya kiislamu inayohusiana na mfumo wa maisha ya binadamu ya kila siku ili kutekeleza vipengele vya dini.

b) Misingi ya Fiqh inayotegemeana

i) Qur'an, hii hutegemea sunnah ili kuweza kuka milisha ujumbe wake. Kwa hiyo ili kukamilisha lengo inatakiwa kutekeleza sunnah.

ii) Sunnah, pia sunnah hutegemea Qur'an katika kufikisha ujumbe kwa sababu Qur'an ndiyo muongozo wa maisha ya mwanadamu.

iii) Ijtihad, pia ili kufanya ijtihad unapaswa kuka milisha Sunnah na hadith na hii inamaanisha ambayo ni ~~Ijma~~ Qiyas na ijma'i.

Kielelezo namba 7.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 7

### 2.2.6 Swali la 8: Sunnah na Hadithi

Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b), katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza maana ya Hadithi sahihi na kipengele (b) alitakiwa kutaja vigezo vinne vya Hadithi sahihi kwa kuzingatia matini yake.

Watahiniwa 62,911 (92.7%) kati ya 67,876 (100%) walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 55,833 (88.7%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 6,261 (10.0%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 817 (1.3%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na 8 inaonesha ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 8:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, asilimia 88.7 sawa na watahiniwa 55,833 walitapa alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao watahiniwa 38,020 (56.0%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu. Baadhi ya watahiniwa hawa waliacha kujibu swali hili na wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sunnah na Hadithi, hivyo walishindwa kubaini majibu sahihi. Aidha, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefafanua zaidi sababu za watahiniwa hao kupata alama za chini.

Katika kipengele (a) baadhi ya watahiniwa walifafanua maana ya Hadithi sahihi kuwa; *Hadithi sahihi ni hadithi iliyoandikwa kipindi cha maswahaba,* na wengine walijibu: *Hadithi sahihi ni zile ambazo zilihakikiwa kabla ya kuandikwa.* Mtahiniwa mwingine alijibu: *Hadithi sahihi ni mapokez*i, na mtahiniwa mwingine alijibu kuwa: *Hadithi sahihi ni zile Hadithi zilizoandikwa na kuchapishwa na Mtume Muhammad* (s.a.w) *enzi za Maswahaba.* Majibu yote yaliashiria kutokuwa na maarifa juu ya dhana ya Hadithi sahihi badala yake walitoa maoni yao ambayo hayakuwa sahihi.

Katika kipengele (b), baadhi ya watahiniwa walitaja vigezo vya Hadithi sahihi kuwa, (i) *Iwe imekamilika kabla ya kuandikwa*, (ii) *Iende kinyume na muongozo wa Allah* (iii) *Isipingane na sharia na kanuni za Allah*. Ingawa

hoja ya (iii) ilikuwa na sehemu ya usahihi lakini ilipingana na hoja ya (ii). Hali iliyoonesha kuwa majibu hayo yalitokana na maoni binafsi ya mtahiniwa ambayo kwa ujumla hayakuwa sahihi.

Mtahiniwa mwingine aliandika sehemu za Hadithi kamili ambazo ni: *Iwe na Isnad, Iwe na matini na Iwe na Rawi,* Wengine waliandika aina za Hadithi kama vile; *Hadithi Nabawiy, Hadithi qudusiy, Hadithi Hassan na Hadithi dhaifu*, na baadhi yao walitaja vitabu vya Hadithi na waandishi kama vile: *Sahihi bukhari, Sahihi Muslim, Wasimulizi wa Hadithi na Waandishi wa Hadithi*. Majibu haya yalikosa vigezo sahihi vya kupima matini.

Mbali na hao, watahiniwa wengine walibuni vigezo vyao bila kuakisi vigezo vya matini. Vigezo walivyoviandika ni: (i) *Hadithi sahihi iwe imeandikwa na Mtume (s.a.w),* (ii) *Hadithi sahihi ielezee historia ya maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w),* (iii) *Hadithi sahihi iwe inaelezea ukweli juu ya uislamu na* (iv) *Hadithi sahihi iwe inaelezea maamrisho na makatazo ya Allah (s.w)*. Kwa ujumla watahiniwa hawa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu uchambuzi wa Hadithi. Hivyo walipata alama hafifu au 0. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


8. a) Hadithi sahihi ni hadithi ambayo aliyoleta mtume (s.a.w) ili kuwapa fundisho wanadamu.
b) i) kuwaelimisha watu
ii) kuwatoa watu kwenye giza na kuwapeleka kwenye mwangaza.
iii) kumpwekesha Allah (s.w) na mtume wake (s.a.w)
iv) kumsaidia mja kuelewa anachokifanya.

Kielelezo 8.2 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.

Watahiniwa 7,078 (11.3%) waliofaulu katika swali hili na kupata alama kuanzia 2 hadi 5, waliashiria kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sunnah na Hadithi hususani katika uchambuzi wa Hadithi sahihi. Watahiniwa hao walifafanua dhana ya Hadithi sahihi na kuandika vigezo vinavyozingatiwa katika kuhakiki Matini ya Hadithi. Kati yao watahiniwa 6,261 (10.0%) walipa alama za wastani (2 hadi 3.5). watahiniwa hawa walijibu kipengele cha kwanza (a) na kuandika hoja mbili sahihi katika

kipengele (b). Wengine walishindwa kutoa maana ya Hadithi sahihi katika kipengele (a) na kutaja vigezo vitatu sahihi katika kipengele (b). Hivyo, walipata alama za wastani katika swali hili.

Aidha, watahiniwa 817 (1.3%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika uchambuzi wa Hadithi. Hivyo walitaja vigezo sahihi vinavyotumika kuhakiki matini ya Hadith. Katika kipengele (a) watahiniwa hao walieleza kwa ufasaha dhana ya Hadithi sahihi kuwa ni: *Hadithi ambayo haina dosari katika sanad wala katika matini na imethibitishwa hivyo na wanazuoni.*

Katika kipengele (b) walitaja kwa usahihi vigezo vinavyopima matini ya Hadithi sahihi kuwa ni: (i) *Haipingani na aya yoyote katika Qur'an,* (ii) *Haipingani na Hadithi nyingine iliyothibitishwa kuwa ni sahihi,* (iii) *Haitoi adhabu kubwa kwa kosa dogo,* (iv) *Haitoi ahadi kubwa ya malipo kwa amali ndogo na* (v) *Haipingani na ukweli wa kimazingira.* Kielelezo Na 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.


8 a) Hadith sahihi. Ni hadithi isiyo na
mapungufu yoyote yale ya matini na
wasimulizi wake hawana kasoro.

b) i). Matini yake isimzulie Mtume uwongo.
ii). Isiahidi malipo makubwa kwa jema dogo
na adhabu kubwa kwa ovu dogo.
iii) Iendane na hakika (fact).
iv) Isipingane na Qur-an.
v) Isipingana na hadith iliyothibitika
kuwa ni sahihi.

Kielelezo Na. 8.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8

### 2.2.7 Swali la 9: Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada.

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleze namna ambayo mwanaadamu atalitekeleza lengo la kuumbwa kwake, ambapo jumla ya watahiniwa 64,902 (95.6%) kati ya watahiniwa 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu walijibu. Kati ya watahiniwa hao 31,012 (47.8%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5), 30,092 (46.4%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 3,798 (5.9%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 9:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa, asilimia 52.2 sawa na watahiniwa 33,890 walitapa alama 2.5 hadi 5. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wastani. Majibu ya watahiniwa hawa hayakufafanua nyanja zote za maisha ya mwanadamu kulingana na upana wa dhana ya Ibada katika Uislamu. Hivyo walipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 3,798 (5.9%) walipata alama za juu (4 hadi 5). Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Ibada katika mtazamo wa Uislamu. Hivyo walifafanua kwa ufasaha namna ambavyo mwanadamu ataweza kutekeleza lengo la kuumbwa kwake. Watahiniwa hao walijibu kuwa; *Mwaanadamu atalitekeleza lengo la maisha yake kwa kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii kwa kuzingatia sheria za Allah (s.w) katika muda wake wote wa*

*masaa 24 na katika maisha yake yote kama alivyotuelekeza Mwenyezi Mungu (s.w) katika Qur'an (3:191)*. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha mfano wa jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


9 ⇒ Mwanadamu ataweza kutekeleza lengo la kuumbwa kwake kwa kufuata na kutekeleza sheria na nguzo zote alizoziamrisha mwenyezimungu na kwa cha yale yote aliye yakataza katika maisha yake yakila siku yakibinafsi na yakijamii.

Kielelezo 9.1 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 9

Uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa umebaini kuwa, watahiniwa 31,012 (47.8) walipata alama hafifu (0 hadi1.5). Watahiniwa hao walijibu tofauti na matakwa ya swali kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha juu ya dhana ya Ibada katika Uislamu. Aidha, kati ya watahiniwa hao, 16,818 (24.8%) walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hao waliacha kujibu swali na wengine walishindwa kutoa majibu sahihi ya swali.

Miongoni mwa watahiniwa walioshindwa kuelewa matakwa ya swali hili, walieleza utekelezaji wa nguzo tano za Uislamu kama vile: *Kusimamisha swala tano, kutoa zaka, kufunga mwezi wa Ramadhani na kwenda kuhiji makka kwa mwenye uwezo.* Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa, kutekeleza nguzo za Uislamu ni sehemu ndogo katika kutekeleza lengo la kuuumbwa kwa mwanadamu.

Wengine walieleza kuwa, *Lengo la kuumbwa hutekelezwa kwa kuamini Nguzo za Imani ambazo ni kuamini Allah, kuamini malaika wa Allah, kuamini vitabu vya Allah, kuamini Mitume wa Allah na kuamini siku ya Mwisho.* Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa vema dhana ya nguzo za Imani ya Kiislamu. Kwani nguzo hizo zinasimama kama msingi wa kiitikadi katika kuliendea lengo kuu la kuumbwa kwa mwanadamu.

Kwa ujulma majibu mengi yaliyotolewa na watahiniwa waliopata alama za chini hayakutosha kueleza kwa ukamilifu dhana ya utekelezaji wa lengo la kuumbwa kwa mwanadamu. Hii ni kwa kuwa yalikosa kuzingatia nyanya zote za maisha ya mwanadamu kama ilivyo dhana ya Ibada katika Uislamu. Kielelezo namba 9.2 kinaonyesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 9.



9. Kumuabudu mwenyezimungu
Kutekeleza ibada kwa wakati
Kusoma kitabu chake kitukufu Qur-an
Kumuamini muhammad (s.a.w)
Kuamini mitume ya Allah.
Kufanya yale yaliyomema katika dunia

Kielelezo Na. 9.2 Sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali la 9.

Katika kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa ameorodhesha baadhi ya nguzo za Imani ya Kiislamu badala ya kufafanua namna ya kutekeleza lengo la kuumbwa kwa mwanadamu.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne ya insha. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu kati ya hayo. Maswali yalitoka katika mada za *Nguzo za Uislamu, Mtazamo wa uislamu juu ya Elimu, Qur'an na Historia katika Uislamu.* Kila swali lilikuwa na alama 15 hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 45.

### 2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha tofauti nne kati ya Funga ya Ramadhani na Funga za Sunnah. Aidha, watahiniwa 65,284 (96.2%) kati ya 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 34,038 (52.1%) walipata alama za chini (0 hadi 4.5). Watahiniwa 27,110 (41.5) walipata alama za wastani (5 hadi 9.5) na watahiniwa 4,136 (6.3%) walipata alama za juu (10 hadi 15). Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 10.*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa, asilimia 52.1 sawa na watahiniwa 34,038 walitapa alama za chini (0 hadi 4.5), kati yao watahiniwa 4,121 (6.1%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa imeonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha sababu mbalimbali za watahiniwa hao kupata alama za chini kama ifuatavyo:

Baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu wa chini walieza sifa za Funga ya Ramadhani na kuandika kinyume chake kwa upande wa Funga za Sunnah. Watahiniwa hao walieleza kuwa; (i) *Funga ya Ramadhani humfanya mja kuwa mkarimu wakati Funga za Sunnah huwanyenyekeza waja mbele ya Allah (s.w) hapa duniani, (ii) Funga ya Ramadhani humfanya mja kuwa na subira pale ambapo atakapokuwa amepatwa na jambo la kuhuzunisha wakati funga za Sunnah humfanya mja kutokuwa na subira pale ambapo atakapokuwa amepatwa na shida, (iii) Funga ya Ramadhani humfanya mja kuwa na Huruma wakati funga za Sunnah humfanya mja kutokuwa na Huruma, (iv) Funga ya Ramadhani humfanya mja kuwa na hekima wakati funga za Sunnah haziwezi kumfanya mja kuwa na hekima.* Hoja hizi hazikuwa sahihi kutofautisha baina ya Funga hizo bali baadhi yake ni athari zinazopatikana katika Funga yoyote.

Wengine walieleza faida za Funga ya Ramadhani na Funga za Sunnah badala ya kutofautisha. Faida walizotaja ni pamoja na (i) *Funga ya Ramadhani humfanuya mja kuwa ni mwenye afya,* (ii) *Funga ya mwezi wa*

*Ramadhani humfanya mja kuwa ni mcha Mungu,* (iii) *Funga ya mwezi wa Ramadhani humfanya mja kutotenda maovu na machafu,* (iv) *Funga za Sunnah humfanya mja kujiandaa na funga za Ramadhani,* (v) *Funga za Sunnah humfanya mja kukiri makosa yake.*

Kwa ujumla watahiniwa hawa hawakuweza kujenga hoja zinazotofautisha baina ya Funga za Sunnah na Funga ya Ramadhani. Hivyo baadhi yao walipata alama hafifu na wengine walipata alama 0. Kielelezo namba 10.1 kimeonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha kati ya Funga ya Ramadhani na Funga za Sunnah.



10: Kubainisha tofauti nne kati ya Funga ya Ramadhani na Funga za sunnah.

| | Funga ya Ramadhani | Funga ya sunnah |
|---|---|---|
| i: | Inafunguwa kwa mwezi mala moja | Unafunga kwa ~~ktaa~~ siku yeyote unayotaka kufunga |
| ii: | Ina sharti zake zakufunga | Nayo inasharti zake zakufunga |
| iii: | Unafunga kwamda mufaka naunafunguakwa mdamufaka. | Unafunga kwa mdamu afana unafungua kwamda muwafaka |
| iv | Ni lazima kufunga isipokuwa kwa wenye udhulu | Si lazima ni sunah ukitaka kufunga. |

Kielelezo 10.1 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 10.

Katika kielelezo Na. 10.1 mtahiniwa alishindwa kujibu swali kwa muundo wa insha na kuandika hoja zake kwa jedwali ambapo pia hakuweza kutoa hoja sahihi isipokuwa hoja moja tu ya (iv) ambayo haikuwa na maelezo yanayojitosheleza.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 31,246 (47.9%) walifaulu katika swali hili kwa kupata alama 5 hadi 15. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa kuhusu Funga na walielewa mahitaji ya swali. Kati yao watahiniwa 27,110 (41.5%) waliopata alama za wastani (5 hadi 9.5) baada ya kushindwa kubainisha tofauti zote nne kati ya Funga ya Ramadhani na Funga za sunnah. Baadhi yao walitoa sifa za Funga ya Ramadhan bila kuonesha tofauti zake na Funga za Sunnah hivyo hoja zao hazikutosheleza kuonesha tofauti baina ya ibada hizo. Hatimaye walipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 4,136 (6.3%) waliopata alama za juu, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Funga na walielewa vema mahitaji ya swali hilo. Hivyo, waliweza kubainisha kwa ufasaha tofauti zilizopo baina ya Funnga za Sunnah na ile ya Ramadhan. Watahiniwa hao walionesha tofauti kwa hoja zifuatazo: (i) *Funga za Sunnah hutekelezwa na waumini katika nyakati mbalimbali za mwaka kwa mujibu wa maelekezo ya Mtume(s.a.w) wakati Funga ya Ramadhani ni funga ambayo imefaradhishwa katika mwezi wa Ramadhani na hutekelezwa ndani ya mwezi huu tu,* (ii) *Nia ya Funga ya Ramadhani ni lazima iletwe kabla ya kuingia alfajiri ya siku ya funga wakati nia ya swaum ya Sunnah inaweza kuletwa hata kama jua limeshatoka madhali mtu hajafanya lolote katika yanayobatilisha funga,* (iii) *Funga za Sunnah inaweza kuvunjwa wakati wowote pasi na sababu yoyote ya kisheria wakati funga ya Ramadhani haiwezi kuvunjwa wakati wowote pasi na sababu ya kisheria,* (iv) *Ni lazima kulipa funga ya Ramadhani ukipatwa na dharula kama vile ugonjwa, safari na kwa wanawake kupatwa na Hedhi au nifasi kwa upande wa funga za Sunnah muumini anaweza kuikatiza funga au kutofunga na hatowajibika kuzilipa siku alizoacha* na (v) *Funga ya Ramadhani ni katika nguzo za Uislamu kinyume na funga za sunnah.* Kielelezo Na 10.2 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa aliyeweza kutofautisha vizuri kati ya Funga za Sunnah na Ramadhani.

10. Funga:- Ni kujizuilia kufanya jambo, ambapo kisheria ni kujizuilia kula na kunywa na vyote vinavyobatilisha funga kuanzia kuchomoza kwa jua hadi kuzama magharibi (kuzama kwa jua). Funga huweza kuwa ya faradh ambayo ni ya ramadhani tu na funga za - Sunnah ambazo huweza kuwa kama vile:- funga ya Ashura na Arafa. Zifuatazo ni tofauti kati ya funga ya Ramadhani na funga za Sunnah:-

Funga ya ramadhani ni ya lazima (Faradhi) lakini funga za Sunna si lazima:- kwa muislamu ambaye hana dharura za kumzuilia kufunga ni lazima kwake kufunga ramadhani ili - aweze kwa mchamungu na kutekeleza - nguzo ya nne ya uislamu wakati funga za Sunnah mtu akiacha kufunga hawezi kupata dhambi. Mfano:- kuacha kufunga Arafa.

Funga ya ramadhani nia hunuiwa kabla ya kutokea weupe wa Alfajiri lakini nia za funga za Sunna ni muda wowote:- muislam hutia nia yake usiku kabla ya kupambazuka asubuhi / kuchomoza kwa jua na ni lazima kwake kufunga lakini nia ya funga za Sunnah hunuiwa muda wowote na sio lazima funga hiyo kuitekeleza. Mfano:- Imethibiti kwa mtume (S.a.w) kuwa alifunga baada ya kuletewa chakula akisimuliwa Aisha (r.a).

Funga ya ramadhani hufungwa katika - mwezi wa ramadhani kama kielelezo cha kushuka Qur'an:- lakini funga za sunnah hufungwa kwa siku tu ambapo sio kiele- lezo cha kushuka kwa Qur'an Tukupe

10. bali kupata thawabu tu na hivyo funga ya ramadhani kuwa na hadhi na daraja kubwa kuliko zile za Sunnah. Mfano:- Anayefunga ramadhani huesabiwa siku kumi na hupewa daraja la pepo.

Nguzo ya Uislamu ya nne ni funga ya ramadhani lakini funga ya Sunna si nguzo ya Uislamu:- Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano, na nguzo ya nne ni kufunga mwezi mtukufu wa ramadhani ambaye mtu anayeacha bila ya dharura anaukanusha uislamu, lakini anayeacha funga ya sunnah haukanushi Uislamu. Mfano:- Mtu anayekula kwa makusudi mchana wa ramadhani hawezi kulipa hata akifungwa mwaka mzima.

Kwa Ujamla:- Ibada zote za funga zinampelekea mja kuwa katika uchamungu kama Allah (s.w) anavyosema katika Suratul Baqara "Mumelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa kufunga kabla yenu ili mpate kuwa wachamungu" hivyo waislamu hatuna budi kujipamba na Sunnah na faradh ili tupate kufuzu.

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 10.

### 2.3.2 Swali la 11: Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuthibitisha kwa kutumia hoja tano kuwa Uislamu unasisitiza utafutaji wa Elimu. Kati ya watahiniwa 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu, Watahiniwa 55,591 (81.9%) walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 47,794 (86.0%) walipata alama hafifu (0 hadi 4.5). Watahiniwa 7,196 (12.9) walipata alama za wastani (5.0 hadi 9.5) na watahiniwa 601 (1.1%) walipata alama za juu (10.0 hadi 15.0). Chati Na. 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 11:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, asilimia 86.0 sawa na watahiniwa 47,794 walipata alama hafifu (0 hadi 4.5). Kati yao watahiniwa 13,263 (19.5%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa inaonesha kuwa kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa dhaifu. Watahiniwa hawa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya elimu katika Uislamu. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefafanua zaidi sababu za watahiniwa hawa kupata alama za chini kama ifuatavyo:

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umebaini kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu hawakujibu hoja ya swali badala yake waliandika hoja tofauti ambazo ni maoni yao. Hii iliashiria kuwa watahiniwa hawa walielewa vibaya swali na wengine hawakuwa na maarifa sahihi juu ya dhana ya elimu kwa mujibu wa Uislamu.

Baadhi ya watahiniwa hawa walijenga hoja kuwa, *Elimu ya akhera inasaidia watu kuepukana na mambo maovu na machafu, Elimu ya akhera hutusaidia kujua umuhimu wa kumuabudu Allah, Elimu ya muongozo humsaidia mtu kuchuma chumo lililo halali.na Elimu ya mazingira husaidia kuinua pato la Taifa.* Majibu haya yanaashiria kueleza faida za elimu badala ya kuthibitisha kama Uislamu unasisitiza kutafuta elimu.

Mtahiniwa mmoja aliorodhesha baadhi ya vipengele vinavyoashiria kueleza dhana ya Dini badala ya elimu, kama vile: *Kutafuta dini iliyo sahihi, Vipaji vya mwanadamu juu ya dini, kufundishwa na kuelimishwa*

*kwa dini na umbile la mwanadamu katika dini*. Hoja hizi zilijikita katika kueleza dhana ya Dini badala ya kuthibitisha utafutaji wa Elimu kama ambavyo swali lilihitaji.

Wengine walijibu kuwa, (i) *Adhabu kwa wasiotafuta elimu,* (ii) *Ili uutambue na uujue uislamu inakubidi usome vitabu mbali mbali ili uukamilshe uislamu na* (iii) *Mitume wa Mwenyezi Mungu walikuwa na Elimu ambayo iliwasaidia kulingania dini ya Allah (s.w).* Majibu hayo hayathibitishi kuwa Uislamu unasisitiza utafutaji wa Elimu bali yanaeleza athari za elimu kwa ujumla.

Kwa muhtasari, hoja nyingi zilizotolewa na watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi, hazikuwa na uhusiano na dhana ya elimu katika Uislamu. Aidha, majibu yao yalionesha kuwa walikosa ufahamu juu ya mada hiyo. Hivyo baadhi yao walipata alama hafifu na wengine walipata alama 0. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa aliyejibu swali hili.

11 Elimu ni jambo lamuhimu sana kwa mwanadamu katika kuyafikia yale malengo ya kuumbwa kwake katika hii dunia au inalazimu kila mwanadamu kutafuta elimu kama tulivyo amrishwa na Allah (sw) na mtume wake.

Ili kumpwekesha Allah (sw). Mtu mwenye elimu ndiye ambaye anaweza kumpwekesha Allah (sw) kwa sababu ataкuwa anamjua na kuweza kumfanyia ibada zake kwa ukamilifu bila hata ya kumshirikisha kwa sababu watu ambao hawajasoma hawawezi kumpwekesha Allah (sw) na kuweza kumshirikisha tu.

Ili kuwa khalifa au kiongozi katika jamii. Dini ya kiislamu ina sisitiza watu wapate elimu ili waweze kuwa viongozi katika jamii zao na kutoa elimu katika jamii zao maana ili uwe kiongozi mwadilifu lazima uwe na elimu ya kuweza kuwaongoza watu katika jamii

Ili kuamrisha yaliyo mema na kukataza maovu. Mtu mwenye elimu ndiye anaye weza kujua mambo mema yanayotendeka katika jamii na mambo maovu yanayo tendeka katika jamii ili uweze kuamrisha yaliyo kuwa mema na kukataza mambo maovu katika jamii unahitajika uwe na elimu ambayo itakupeleka kujua yalio mema na kuyakataza maovu.

Ili kuweza kulinda mazingira. Mtu aliye kuwa na elimu ndiye mwenye uwezo wa kuya hifadhi na kuya tunza madhingira kutokana na vitu vinavyo weza kuleta hathari za madhara mabaya katika madhingira kutokana na hayo ni muhimu kuwa na elimu ili kuweza kulinda mazingira.


11 Ili kusimamia Sharia na hukumu za Allah(s.w)
katika jamii. Ili mtu aweze kusimamia Sharia
na hukumu za Allah (S.w) katika jamii ina
mlazimu asome ili aweze kuwa na elimu ambayo
yo itamuwezesha katika kusimamia Sharia na
hukumu za Allah S.w katika jamii
Suala la elimu katika uislamu ni jambo la
muhimu sana ili watu waweze kumuabudu na
kumpwekesha Allah (S.w) lazima wawe na elimu na
pia suala la uongozi lina hitaji watu wenye elimu
ili waweze kuongoza uzuria katika jamii

Kielelezo Na. 11.1 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, watahiniwa 7,797 (14.0%) walifaulu katika swali hili na kupata alama 5 hadi 15. Kati yao watahiniwa 7,196 (12.9%) walipata alama za wastani (5.0 hadi 9.5). Watahiniwa hawa waliandika hoja sahihi za majibu lakini walishindwa kuzifafanua hoja hizo. Wengine walitoa hoja pungufu ya nne na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo walipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 601 (1.1%) waliopata alama za juu, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya elimu kwa mujibu wa Uislamu na walielewa vema mahitaji ya swali hilo. Watahiniwa hawa waliweza kuthibitisha namna ambavyo Uislamu unasisitiza watu kutafuta elimu kwa hoja sahihi na kwa ufasaha. Hoja walizotumia watahiniwa hawa ni pamoja na: *Elimu ndiyo jambo la kwanza ambalo Allah(s.w) alimpa Nabii Adam(a.s) baada ya kumuumba,* (ii) *Ni amri ya kwanza aliyopewa Mtume(s.a.w) na waumini kwa ujumla,*(iii) *Elimu ndiyo njia pekee ya kufikia uchamungu,* (iv) *Qur'an imewatukuza watu wenye Elimu dhidi ya wasiokuwa na Elimu,* (v) *Qur'an imetufahamisha kuwa waumini waliobobea kwenye Elimu wana daraja kubwa Zaidi na* (vi) *Mafundisho mbalimbali ya Mtume yanasisitiza juu ya utafutaji wa Elimu katika fani mbalimbali zenye manufaa katika jamii.* Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.

11. Elimu ni ujuzi ulioambatanishwa na utendaji. Kutafuta elimu uislamu unasisitiza sana kwamba kila muislamu anatakiwa akatafute elimu. Zifuatazo ni sababu zinazopelekea kwa uislamu kusisitiza wa utafutaji wa elimu;

Elimu ndiyo jambo la kwanza alilo ~~ambiwa~~ ~~teremshiwa~~ amrishwa Mtume Muhammad (s.a.w) kutoka kwa mola wake. Mtume jambo la kwanza kuamrishwa na mola wake ni kuhusu elimu ambapo zilishuka aya tano ambazo ni "Iqraa bi

اِقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ، خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ

اِقْرَأْ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ، عَلَّمَ الْإِنْسَانَ

مَا لَمْ يَعْلَمْ.

Tumeamrishwa na Allah (s.w) tutafute elimu ili tuweze kumfahamu yeye zaidi. Mwenyezimungu anatuambia kwamba tutafute elimu ili tuweze kumfahamu ~~yeye~~ Allah (s.w) kwa sababu fani zote za duniani zinatokana na Allah wengine hao ni sababu tu. Kwa hiyo tuna sisitizwa kutafuta elimu ili tuweze kusimamisha dini katika jamii.

Mbora mbele ya Allah ni yule mwenye elimu kuliko yule ambaye hana elimu. Wanaadam tumeumbwa ili tuje kuwa makhalifa wa hapa ulimwenguni ili tuje tusimamishe uislam katika jamii. Lakini haiwezekani kuwa khalifa kama hakuna elimu kwa sababu hata mtume mwenyewe ili aweze kusimamisha uislam zaidi lazma asome. Kwa hiyo uislam unasisitiza kutafuta elimu kwa sababu mbora mbele ya Allah (s.w) ni yule mwenye elimu.

Elimu humuwezesha mwanaadamu kutenda mambo yake kwa ufanisi zaidi. Uislamu unasisitiza utafutaji wa elimu kwa sababu mtu aliye elimika ni tofauti na asiye elimika kwa sababu mtu aliye elimika huweza kutenda mambo yake kwa ufanisi zaidi mfano katika Qur'an m'mungu anatuambia

هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

Kutafuta elimu ni faradhi kwa kila muislamu. Faradhi ni jambo la lazima kulifanya na wala sio hiari kwa hiyo uislamu unasisitiza utafutaji wa elimu kwa sababu utafutaji wa elimu ni lazma kwa kila muislam. Na usipotafuta unapata kuna usemi unasema "elimu itafutwe hata kama ni china" na pia kuna hadithi inasema

"طَلَبُ الْعِلْمِ فَرِيضَةٌ عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ وَمُسْلِمَةٍ"

Hivyo basi waislamu tunasisitizwa kwa sana kila muislamu akatafute elimu ambayo elimu hiyo imegawanyika katika elimu ya mazingira na ya muongozo na hata hivyo pia elimu inamanufaa makubwa sana kwa mwanaadam kama atasoma kwa lengo la kumuabudu Allah (s.w).

Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 11.

### 2.3.3 Swali la 12: Qur'an

Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b). Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kuonesha hatua tatu alizochukua Mtume (s.a.w) katika kuihifadhi Qur'an kimaandishi. Na kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kutoa sababu ya kunakiliwa upya kwa Qur'an wakati wa Khalifa Uthman (r.a). Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 19,091 (28.1%) kati ya watahiniwa 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu. Hivyo basi, watahiniwa 17,489 (91.6%) walipata alama hafifu (0 hadi 4.5). Watahiniwa 1,393 (7.3%) walipata alama za wastani (5.0 hadi 9.5) na watahiniwa 209 (1.1%) walipata alama za juu (10 hadi 14.5). Chati Na. 12 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 12**: *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa, asilimia 91.6 sawa na watahiniwa 17,489 walipata alama hafifu (0 hadi 4.5). Kati yao watahiniwa 8,995 (13.3%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa inaonesha kuwa kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu.Watahiniwa hawa walikosa maaarifa ya kutosha katika historia ya kuandikwa kwa Qur'an. Majibu ya watahiniwa hao yalitofautina kulingana na vile walivyojaribu kueleza na kuunganisha matukio. Aidha, uchambuzi umebainisha sababu mbalimbali za ufaulu huo kama ifuatavyo.

Katika kipengele (a) baadhi ya watahiniwa waliandika sehemu ambazo Mtume (s.a.w) na maswahaba (r.a) walihifadhia Qur'an kama vile, *Alihifadhi kwenye magome ya miti, Alihifadhi kwenye ngozi za wanyama na alihifadhi kwenye makuti ya mtende.* Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa mujibu wa swali pia yalionesha kufahamika vibaya kwa historia ya uandishi wa Qur'an.

Watahiniwa wengine ambao walishindwa kuelewa matakwa ya swali hili, waliandika sababu zilizopelekea kuhifadhiwa Qur'an kama vile: *Ili waweze kuielewa, ili iweze kuhifadhika katika nyoyo zetu na ili waweze kuisoma na kuandika*. Majibu haya yalionesha kueleza malengo au sababu za kuhifadhiwa kwa Qur'an na siyo namna ilivyoandikwa.

Baadhi ya watahiniwa walionyesha hatua tatu za jumla za kuhifadhiwa Qur'an ambazo ni: *Qur'an kuhifadhiwa kifuani kwa mtume, Qur'an kuhifadhiwa kifuani mwa maswahaba na Qur'an kuhifadhiwa katika*

*maandishi*. Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa, swali lilihitaji hatua tatu mahususi za kuihifadhi Qur'an kimaandishi.

Katika kipengele (b) miongoni mwa watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi waliandika; *Qur'an ilinakiliwa upya katika kipindi cha khalifa Uthman kwa sababu walimzulia Mtume hadithi za uongo*. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa kuzuka kwa Hadithi za uongozo ni jambo ambalo halikuhusiana na kunakiliwa upya kwa Qur'an.

Watahiniwa wengine walitoa hoja kuwa, *kuifanya Qur'an kuwa ni kitabu cha hukumu na kuiepusha Qur'an na kuibadilisha na makafiri*. Hoja hii ilionesha kuwa, mtahiniwa huyo hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Qur'an, kwani Qur'an ni kitabu kilicho na ahadi ya ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w). Aidha mtahiniwa mwingine alijibu kuwa, *Qur'an ilinakiliwa upya wakati wa khalifa Uthman kwa sababu uhitaji wa Qur'an ulikithiri sana wakati wa Sayyidina Uthman na hivyo aliamru inakiliwe tena ili itoe msaada kwa watu, Utajiri wa uthman (alikuwa na pesa ya kuwalipa waandishi wa Hadithi), Chokochoko ya madai ya makafiri dhidi ya Qur'an na Ili isambazwe kwa waumini waislamu na washirikina*. Hoja hii pia haikuwa sahihi kwa kuwa ilipingana na sababu za kihistoria.

Majibu hayo ya watahiniwa kwa ujumla yaliashiria kutofahamika vema kwa historia ya Qur'an. Hivyo, watahiniwa hao walishindwa kubaini hoja sahihi za swali na hatimaye walipata alama hafifu na wengine alama 0 kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 12.2.

12 Mtume (s.a.w) alichukua hatua mbalimbali katika kuhifadhi Qur'an kimaandishi. Hatua hizo ni zifuatazo :-

Aliihifadhi kwenye Magome ya miti. Mtume (s.a.w) alisaidiana na Maswahaba kuhif adhi Qur'an kwenye magome ya miti ambapo Qur'an hiyo waliita vifuni mwao. Miti hiyo ilikuwa mmoja wapo ni Mtende waliihifadhi hapo.

Aliihifadhi kwenye Ngozi za wanyama kwakukosa sehemu ya kuandikia mfano karatasi kwa wakati huo waliamua kuihifadhi kwenye ngozi za wanyama mfano Ng'ombe, Mbuzi, kondoo, Ngamia nk.

Aliihifadhi kwenye makuti ya mtende Mti hu hupatikana sana kwenye bara arabu kwa sababu nimoja kati ya miti inayoweza kustahamili hali ya ukame pia Mtume (s.a.w) na Maswahaba zake waliiandika Qur'an kwenye matawi ya mti huu ambao ni Mtende.

Pia Qur'an ilinakiliwa upya wakati wa khalifa Uthman (r.a) kwa sababu zifuatazo :-

kuifanya au kuiweka Qur'an kwenye kitabu kimoja. Kabla ya kukusanywa zilikuweko kurasa nyingi zilizokuwa zimeandikwa Qur'an hivyo khalifa Uthman (r.a) aliamua kuzikusanya na kuzinakili upya kwenye kitabu kimoja ambacho ni Mas-haf.

kuifanya Qur'an kuwa kitabu cha hukumu. Qur'an yenyewe imebeba kila kitu ili kuipata vitu hivyo Qur'an ilibidi inakiliwe upya na sura zipangiliwe ili iweze kueleweka ipasavyo kwa mujibu wa mtiririko wake maalum.


12. kuipesha Qur'an na kubadilishwa na makafiri. kwa wakati huo makafiri waliiandama dini ya kiislamu pamoja na viashiria vyake moja ya viashiria hivyo ni Qur'an hivyo Khalifa Uthman (r.a) aliinakili upya ili aweze kuilinda au kuongeza ulinzi zaidi dhidi ya makafiri japokuwa Allah (s.w) Aliahidi kuilinda Qur'an dhidi ya wale hao.
Hizo ni baadhi ya njia ambazo Mtume (s.a.w) alizitumia kuandika au kuhifadhi Qur'an kwa njia ya Maandishi na hizo ni baadhi ya sababu zilizopelekea kunakiliwa Upya kwa Qur'an wakati wa Khalifa Uthman (r.a).

Kielelezo Na. 12.1 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, watahiniwa 1,602 (8.4%) walifaulu katika swali hili na kupata alama (5 hadi 14.5). Watahiniwa hawa walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa katika mada ya Qur'an. Kati yao watahiniwa 1,393 (7.3%) walipata alama za wastani (5 hadi 9.5). Watahiniwa hawa waliorodhesha hatua alizochukua Mtume (s.a.w) katika kuihifadhi Qur'an kimaandishi, pamoja na sababu za kunakiliwa upya Qur'an wakati wa Khalifa Uthman (r.a) bila ya kuweka ufafanuzi katika hoja zao. Wengine walieleza kwa ufasaha kipengele kimoja na kushindwa katika kipengele kingine.

Aidha, watahiniwa watatu (3) tu miongoni mwa waliofaulu walipata alama 14.5 katika swali hili. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika historia ya Qur'an na waliweza kujibu vipengele vyote kwa ufasaha. Katika kipengele (a) watahiniwa hawa waliweza kuonesha hatua alizochukua Mtume (s.a.w) katika kuihifadhi Qur'an kimaandishi, ambazo ni: (i) *Aliteua waandishi,* (ii) *Waandishi walisoma mbele yake na akahakiki,* (iii) *Mtume (s.a. w) aliwaelekeza waandishi wake wazipange aya na sura sehemu zake kama zilivyo katika msahafu.*

Katika kipengele (b) watahiniwa hao walibainisha sababu zilizopelekea Qur'an kunakiliwa upya wakati wa Khalifa Uthman (r.a), ambazo ni: (i) *kuibuka kwa visomo tofauti ambavyo vilihatarisha kuharibika kwa maana ya Qur'an kutokana na kupanuka kwa dola ya kiislamu katika kipindi cha*

*ukhalifa wake,* (ii) *Kuendelea kufariki kwa maswahaba wengi waliokuwa wamehifahdi na kuifundisha Qur'an kama walivyopokea kutoka kwa Mtume (s.a.w).* Kielelezo Na 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.

12(i) Qur'an: Ni maneno ya allah ambayo
yaliteremshwa kwa mtume ili yawe mwongozo
wa binadamu kwa kupitia kwa Malaika jibril na
mtume alihifadhi maneno hayo katika maandishi ili yaweze
kutumika na kizazi cha mbele bila ya kukosea zifuata
zo ni hatua alizozitumia mtume kuhifadhi Qur'an ka
tika maandishi.

Mtume aliwasomea maswahaba na kuw
aambia waiandike; Mtume baada ya kuhifadhishwa na
malaika jibril mtume aliwahifadhisha maswahaba na
na baada ya kufikiria kwamba Qur'an inaweza ikapotea
mtume aliwasomea maswahaba na kuwaambia waian
dike katika maandishi.

Mtume aliwaambia maswahaba wamsom
ee ili kuhakikisha; baada ya kuandikwa katika ma
andishi mtume muhammadi (s.a.w) aliwaambia ma
swahaba wamsomee hiyo Qur'an ili kuhakikisha
kama imekosewa katika uandishi na kutambua ipo sa
wasawa na haina mashaka.

Kupanga Qur'an katika aya na sura kwa
mtiririko katika mas-hafu; baada ya mtume kuta
mbua na kuridhika kwamba haijakosewa walipanga k
atika sura na aya kwenye kitabu ambacho ni Qur'a
ni na kutumika. Baada ya mtume kufariki na


12 Qur'an kuanza kusomwa na watu wa makabila mba
imbali. wakati wa Khalifa Uthman (r.a) aliinakili Qur
b) an tena. Zifuatazo ni sababu zilizopelekea kunakiliwa
tena Qur'an.
Watu walikuwa wanakosea katika usomaji
wa Qur'an; watu walikuwa wanakosea sana katika
usomaji wa hiyo Qur'an tofauti na mtume muhamm
mad (s.a.w) ambapo ilipelekea Khalifa Uthan kuinak
ili upya Qur an ili watu wasome vizuri.
Ili kuweka hukmu zitakazo mwezesha mtu
kusoma Qur'an vizuri na kwa ufasaha; sababu nyi
ngine ambayo ilipelekea Uthman kunakili upya ni ku
weka hukmu kwa sababu mtume na maswahaba walii
andika Qur'an bila hukmu ambapo makabila mengine
tofauti na waarabu walishindwa kusoma na hukmu hi
zo ni shadda, kisra, fath, zumaa na nyinginezo.
Mwisho; Unakiliji wote huu wa Qur'ani
pamoja na mtume kuhifadhi katika maandishi ili
kuwawezesha waislamu wakizazi kijacho kuikuta
Qur'an na kufuata muongozo wake.

Kielelezo Na. 12.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 12

### 2.3.4 Swali la 13: Historia katika Uislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza madhara watakayopata Waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya Uislamu. Watahiniwa 53,876 (79.4%) kati ya 67,876 (100%) waliofanya mtihani huu walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 40,916 (75.9%) walipata alama hafifu (0 hadi 4.5). Watahiniwa 12,434 (23.1%) walipata alama za wastani (5 hadi 9.5) na watahiniwa 526 (1.0%) walipata alama za juu (10 hadi 15). Chati namba 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 13:** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 13*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa, asilimia 75.9 sawa na watahiniwa 40,916 walipata alama hafifu (0 hadi 4.5). Kati yao watahiniwa 9,276 (13.7%) walipata alama 0. Idadi hiyo ya watahiniwa inaonesha kuwa kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Historia katika Uislamu. Hivyo walishindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili. Aidha, uchambuzi zaidi umefafanua sababu za watahiniwa hao kupata alama za chini kama ifuatavyo:

Baadhi ya watahiniwa waliopata alama hafifu, walijibu kuwa: *Hawatakuwa watu wema, hawataingia peponi, hawatoombewa msaada na Mtume (s.a.w), watakuwa makafiri*. Wengine walijibu kuwa: *kutoijua miji ya kale, Kutojua makaburi ya kale ya waislamu, kutojua miskiti ya kale ya waislamu, kutojua dola ya kiislamu na kujitungia maamrisho yao*. Hoja hizi hazikuwa sahihi kwa sababu hazikubainisha madhara ya msingi ambayo jamii ya Waislamu itapata kwa kutojua Historia ya Uislamu.

Wengine walishindwa kubaini uhusiano wa madhara yanayotokana na kutofahamu Historia ya Uislamu na madhara ya kutofahamu misingi ya Dini. Kwa ujumla watahiniwa hawa walijibu kwa hoja kama vile, *Kutoamini nguzo za Imani na Nguzo za Uislamu*, kama vile: *kutoamini siku ya mwisho, kutoamini uwepo wa Malaika, Kutoamini uwepo wa Mitume, kutotekeleza nguzo za Kiislamu.* Hoja hizi zilionesha kueleza madhara ya

kutofahamu misingi ya Dini kwa ujumla na hazikuwa na uhusiano na madhara ya kutofahamu Historia.

Wapo pia watahiniwa walioshindwa kubaini matakwa ya swali na kueleza dalili zinazothibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu badala ya madhara watakayopata Waislamu endapo hawatajifunza historia yao. Watahiniwa hawa walijibu kama ifuatavyo, *Kutokana na historia ya mwanaadamu, kutokana na historia ya Mitume, Umbile lake, Nafsi ya Mwanaadamu, umbile la mbingu na ardhi na kufa na kufufuliwa kwake.* Majibu haya yaliashiria kueleza hoja zinazothibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu badala ya madhara ya kutoifahamu Historia ya Uislamu.

Majibu yote yaliyotolewa na watahiniwa hawa yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya Dhana ya Historia katika Uislamu. Hivyo, baadhi yao walipata alama hafifu na wengine walipata alama 0. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuzingatia matakwa ya swali.


13 Madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya Uislamu, basi watakuwa ni wenye hasara.
Uislamu katika historia ya Quran imekuwa kuwa ndio dini sahii na hakuna dini isipokua dini ya kiislamu kwa kutumia hoja sita madhara ya watakayapata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya Uislamu inathibitisha kama ifuatavyo,
Kutokana na historia ya mwanaadamu. Mwanaadamu ameumbwa kwa kupitia Udongo, amekuja kwake ni kuja kutekeleza yale alio amrishwa na mola wake.
Kutokana na historia ya Mitume
Mwanaadamu aliletwa kwa kusudio


la kufikisha ujumbe kwa jamii yake
na kutekeleza masharti ya Allah
(s.w) pamoja na Siku ya kurejea kwa-
ke awe amechukua zawadi ya
milele.
Umbile yake. Mwanaadamu ame-
umbwa katika umbile ililobora kabisa
ili aweze kubaliana na Umbile
lake basi ni umbile ambalo unda-
ni kwake linamfahamisha juu ya
kurudi kwa mola wake.
Nafsi ya Mwanaadamu. hii ni katika
Qur-ani imelezwa juu ya nafsi ya
Mwanaadamu kutokana na matendo
yake kupelekea kujitambua yeye kama
yeye.
Umbile la Mbingu na Ardhi.
Mwanaadamu ameumbiwa umbile la
Mbingu na ardhi ili kuthibiti makosa
yake na kufananisha mabaya na
mema kwa kufanya Ibada ya mola
wake na kujifunza mafundisho yalio
bora kwake.
Kufa na kufufuliwa kwake. Mwana-
aadamu ameumbiwa kufa na kufufuli-
wa ili kulipwa kutokana na makosa
na mabaya yake na kupatiwa huku-
mu kwa mema yake na mabaya
yake.
Kwa kutoa kufaulu kwake ataingi-
a katika hasara ilipo kubwa na wawe-
mu wasilewo wanatakiwa kutambua historia
ya uislamu.

Kielelezo 13.1 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 13

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, watahiniwa 12,960 (24.1%) walifaulu katika swali hili na kupata alama kuanzia 5 hadi 15. Watahiniwa hawa walifahamu Historia ya Uislamu na kuelewa matakwa ya swali. Kati yao watahiniwa 12,434 (23.1%) walipata alama za wastani (5 hadi 9.5). Watahiniwa hao walishindwa kutoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu madhara watakayopata Waislamu endapo hawatajifunza historia ya Waislamu. Wengine walibainisha hoja pungufu ya zile zilizohitajika katika swali na wengine waliandika hoja sita kwa kurudia baadhi ya hoja. Wapo pia waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na hatimaye kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 526 (1.0%) pekee walipata alama za juu (10 hadi 15). Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya Historia katika Uislamu na kuelewa vema mahitaji ya swali. Hivyo, walibainisha madhara ambayo Waislamu watapata endapo hawatajifunza

historia ya Uislamu kwa ufasaha. Miongoni mwa madhara hayo ni pamoja na, *Kushindwa kujua asili na hadhi ya mwanadamu juu ya viumbe wengine, kushindwa kukumbuka lengo la kuumbwa kwetu na namna ya kulifikia, Kutojua namna Allah (s.a.w) alivyotuneemesha, Ili tuweze kumuabudu ipasavyo, kushindwa kubaini madhara ya kutofuata muongozo wa Allah(s.w), kushindwa kufahamu namna Mtume na watu wema walivyosimama imara kupambana na dhulma na watawala madhalimu, kukosa fursa ya kujifunza toka kwa kaumu zilizopita na kuchukua tahadhari kabla hayajatufika yaliyowasibu.* Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.

use only

13 Kwa kubainisha hoja sita eleza madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu

Historia ya uislamu ni yale matukio au mambo yaliyofanyika zamani kipindi cha watu wazamani katika maisha yao. yapo madhara watakayo yapata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu. yafuatayo ni madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu

Hawatajua juu ya kumpokea allah (s.w). hii ni moja kati ya madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu. waislamu watapata madhara ya kujua juu ya kumpo kwa allah (s.w) na watashindwa kumuabudu allah (s.w) kuamuabudi viumbe mfano mitimikubwa, mwanamu nawa nyama pia

Kutokujua vipi yalikuja maisha ya mitumi waliopita. Hii ni moja kati ya madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu. kushindwa kujua historia ya mitumi walio pita mfano walikua watu wema waupole na wenye huruma watakuwa wamepata madhara endapo hawatajifunza historia ya uislamu

Hawatajua juu ya lengo la maisha ya hapaulimwengu. Hii ni moja kati ya madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu. kutokujua lengo la kama hawata jifunza historia ya uislamu wakijifunza historia watajua kwa lengo langu hapaulimwenguni ni kumuabudu allah (s.w) na ili kupikia hadhi au cheo chake kikubwa cha ukhalifa

Kutokujua mambo yaliyofanya na watu walio pita na yaka katazwa. Hii ni moja kati ya madhara watakayopata waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu. hawatajua ya li mambo ambayo allah (s.w) amiyakataza na yale ambayo amiya amrishi ya tenda mfano watu walio pita walikuwa wakimshirikisha allah (s.w) na viumbe vyake hawawili visivyo vinikana mfano majini


13 Kutokujua rehma alizotunukia mja allah (s.w) na jinsi ya kuzi
tumia vizuri. Hii ni kati ya madhara watakayopata Waislam wa
leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu mtu atashindwa kujua
rehma alizotunukiwa na allah (s.w) atazitumiaji mfano wa rehma hi
zo ni mali mtu atakapo shindwa kujifunza historia ya uislamu ata
tumia mali zake kwa haramu na atakua amemuasi allah (s.w) laki
ni akijifunza historia ya uislamu atakuwa anatumia kwa njia ili
yo sahihi
Kutokujua mtu atashindwa kujua hatima ya maisha yake
na amri ya allah (s.w) kutokana na yale aliyoyaamrishwa ya kufanya
na yale aliyoyakatazwa. Hii ni moja ya madhara watakayopata
waislamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu mja ata
shindwa kujua hatima ya maisha yake hapa ulimwenguni atakapoji
funza historia ya uislamu atajua kwamba waliokuwa kabla yetu
wametokwa na roho na kurudi kwa allah (s.w)
Kwa ujumla ni kweli yapo madhara watakayopata wai
slamu wa leo endapo hawatajifunza historia ya uislamu. waislamu
wanatakiwa kujifunza historia ya uislamu ili kujua njia sahihi ya
kuishi hapa ulimwenguni na akhira pia kwahiyo waislamu wa
jifunze historia ya uislam

Kielelezo Na. 13.2 Sampuli ya majibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 13

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2020 ulikuwa na maswali kumi na tatu (13) yaliyopima mada kumi na mbili (12). Mada nne (4) kati ya hizo zilipimwa katika swali la kwanza pekee nazo ni; *Tawhiid, Mtazamo wa Uislamu juu ya dini, Imani ya Kiislamu na Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w).* Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa hakuna mada iliyokuwa na ufaulu mzuri, bali watahiniwa walifaulu kwa kiwango cha wastani katika mada tatu (3) pekee ambazo ni; *Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada (52.2%), Nguzo za Uislamu (41.7%)* na *Historia (30.6%).*

Aidha, watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu katika mada za, *Qur'an (25.8%), Fiqh (23.7%), Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu (14.7%), Sunna na Hadithi (11.3%).* Ufaulu wa wastani katika mada zilizotajwa ulichangiwa na ufahamu wa matakwa ya maswali yaliyoulizwa. Hata hivyo watahiniwa hao walishindwa kufafanua hoja walizotoa na wengine kuandika hoja chache katika majibu yao. Aidha, watahiniwa wengine

walichanganya majibu sahihi na dhana zisizokuwa sahihi hivyo walipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa ambao walipata ufaulu hafifu, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizopimwa. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa matakwa ya maswali mengi yaliyopimwa katika mtihani huu. Hivyo hawakuweza kujenga hoja sahihi katika maswali. Muhtasari wa takwimu za uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa kwa ujumla umeoneshwa kwenye Kiambatisho cha pekee ambapo rangi nyekundu imeonesha kiwango hafifu cha kufaulu na rangi ya njano imeonesha kiwango cha wastani.

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika CSEE 2020 somo la Elimu ya Dini ya Kiislaam kilikuwa cha wastani ambapo asilimia 32.71 ya watahiniwa walipata alama za kufaulu. Aidha, uchambuzi umeonesha changamoto mbalimbali ambazo zinapaswa kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo. Changamoto zilizoonekana katika mtihani huu ni pamoja na watahiniwa kutofuata maelekezo ya swali na hatimaye kushindwa kutoa maelezo yanayotosheleza, kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na uelewa mdogo wa mada mbalimbali hasa mada za *Qur'an, Fiqh, Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Sunnah na Hadithi*.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuweza kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu watumie mbinu shirikishi ili wanafunzi wapate nafasi ya kuchangia au kujenga maarifa ili kukuza uwezo badala ya kutumia njia ya kuhubiri.

(b) Walimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu wanapaswa kubadili mbinu za upimaji kutoka maswali ya kupima maarifa pekee na kuhakikisha wanagusa nyanja zote za umahiri.

(c) Wanafunzi wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu wanapaswa kurejea katika vitabu vya kiada katika kujifunza somo la Elimu ya Dini ya

Kiislamu na kujiepusha na maoni yasiyo rasmi ili kuweza kupata hoja sahihi katika dhana mbalimbali.

(d) Wanafunzi wawezeshwe kujifunza kivitendo mada zote zinazowahitaji kutekeleza matendo mbalimbali ya kiibada.

(e) Jitihada zinahitajika kufanywa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika kuwajengea watahiniwa maarifa na uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na namna ya kujenga hoja.

**Kiambatisho cha Pekee**

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA**

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Watahiniwa waliopata alama 30 au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Na. | Ufaulu | | |
| 1 | Sunnah na Hadithi, Tawhiid, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Imani ya Kiislamu, Nguzo za Uislamu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada, Qur'an na Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume hadi Leo. | 1 | 61.7 | 61.7 | Wastani |
| 2 | Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada | 9 | 52.2 | 52.2 | Wastani |
| 3 | Nguzo za Uislamu | 2 | 63.2 | 41.7 | Wastani |
| | | 6 | 13.9 | | |
| | | 10 | 47.9 | | |
| 4 | Historia (Tarekh) | 3 | 37.1 | 30.6 | Wastani |
| | | 13 | 24.1 | | |
| 5 | Qur'an | 4 | 43.1 | 25.8 | Dhaifu |
| | | 12 | 8.4 | | |
| 6 | Fiqh | 7 | 23.7 | 23.7 | Dhaifu |
| 7 | Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu | 5 | 15.3 | 14.7 | Dhaifu |
| | | 11 | 14.0 | | |
| 8 | Sunnah na Hadithi | 8 | 11.3 | 11.3 | Dhaifu |